# *Uzinduzi wa Kiongozi* ©

## *Katabu cha Mwalimu*

Mishale 3 (3 Arrows) — **v4.1 (2024)**

## *“Kupata Uzoefu Wa Agizo Kuu”*

***Strategic Impact***
*S.L.P. 78640, Dar es Salaam, Tanzania*
*www.StrategicImpactInternational.com*
© Haki zote zimehifadhiwa na *Strategic Impact*.
Huruhusiwi kufanya mabadiliko yoyote ya maudhui yaliyomo kwenye kitabu hiki.

# YALIYOMO


**Barua Ya Ukarihisho & Maelezo ya Mwongozo** 3

***Strategic Impact* Maelezo Kwa Ufupi** 5

***Hatua 10 za Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea*** 6

**SESSION OUTLINES** 8

Siku ya 1 (ya Ratiba ya Siku 3)

**Kipindi 1**: Sisi Ni Nani na Kwa Nini Tupo Hapa? 9

**Kipindi 2**: Kuelewa Maono ya Mungu — HAKUNA KIKOMO 12

**Muhtasari**: ***Hatua 10 Za Kuufikia Ulimwengu Uliopotea*** 14

***Hatua 1***: Badili Kufikiri Kwako 16

***Hatua 2***: Omba

***Hatua 3***: Tangaza Maono

**Kipindi 3**: Maono Ya Kiongozi — Kuufikia Ulimwengu Uliopotea 18

***Hatua 4***: Kusanya na Uandae Timu 22

***Hatua 5***: Chagua Mahali

***Hatua 6***: Fanya Unjilisti

**Kipindi 4**: Asili ya Injili: Mafunzo ya Uinjilisti 25

**Zana**: Jinsi Ya kutumia *Mishale 3 Zana ya Tumaini na Maisha ya SI* 27

Siku ya 2

**Kipindi 5**: Kiongozi Anatakiwa Kufanya Nini? 31

**Kipindi 6**: Tabia: Jiwe Kuu la Pembeni la Kiongozi wa Kikristo 33

**Kipindi 7**: Mzigo na Upendo Kwa Ajili Ya Kristo na Waliopotea 35

***Hatua 7***: Wafundishe Wanafunzi Wapya Walioamini 38

**Kipindi 8**: Asili Ya Uanafunzi: Wafundishe Wanafunzi 39

**Zana**: Jinsi ya kutumia *Zana ya Uanafunzi ya Strategic Impact* 40

Siku ya 3

***Hatua 8***: Wakusanye Waamini Wapya 43

***Hatua 9***: Zidisha Wanafunzi 44

**Zana**: Jinsi ya kutumi *Ramani ya Huduma ya Strategic Impact* 46

**Kipindi 9**: Kujitoa Kwa Ajili Ya Agizo Kuu 48

**Kipindi 10**: MWALIKO: *Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea* 50

***Hatua 10***: Fungamanisha Mikono Pamoja ili Kuzindua Mtembeo 53

**Kufunga**: Kufungamanisha Mikono Kwa Ajili Ya Kuweka Agano 54

**Kuzindua *Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea*** 55-62

**Kwa Matumizi Yako** - Jisikie huru kuzalisha tena Zana hizi kwa ajili ya matumizi ya uinjilisti na ufuasi

*Mishale 3 Zana ya Tumaini na Maisha ya SI* 64-65

*Zana ya Ukuaji na Kuzidisha ya SI* 66-67

***Strategic Impact* — Msimamo wa Imani** 68-69

# *BARUA YA UKARIBISHO!*

Wapendwa katika Kristo,

Karibu kwenye *Uzinduzi wa Kiongozi Strategic Impact*! Tunashukuru na tunayo furaha kuona kwamba umefika. Timu yetu imekuwa ikikuombea wewe pamoja na kongamano hili kwa miezi mingi kama sehemu ya maandalizi

Tumeamua kujitenga na majukumu yetu ya kihuduma ya kila siku ili tukae pamoja na tumsogelee Bwana Yesu. Tutacheka pamoja, tutalia pamoja, na tutajifunza pamoja, tutavumbua maeneo ya kujiendeleza/kukua binafsi, kujiendeleza katika uongozi, kujizidisha katika huduma, na mkakati wa *10 Hatua 10 Za Kuufikia Ulimwengu Uliopotea*.

Utawasikiliza wachungaji na wamishenari kutoka nchi mbalimbali na madhehebu tofauti tofauti, vipawa tofauti na viwango tofauti vya uzoefu lakini wanawasha moto wa shauku na mzigo wa kutangaza injili ya Yesu Kristo ili kutimiza Agizo Kuu!

Maombi yetu majira haya ni kwamba Roho Mtakatifu akuhuishe, na udake maono yaliyo wazi kwa ajili ya maisha yako, na huduma, pia utapatiwa mafunzo na zana ili suala la kuzidisha wanafunzi liwe ni jambo la mara kwa mara kama sehemu ya huduma binafsi na wale unaowaongoza. Lakini zaidi ya haya, ni shauku ya mioyo yetu kwamba utapata kiu ya kumtafuta Bwana na Mwokozi wetu.

Katika kongamano hili utatiwa nguvu katika eneo ambalo unahitaji kutiwa nguvu, utatiwa moyo katika maeneo ambayo una mashaka, na utavikwa silaha ili kuendelea kumtafuta Yesu Kristo.

Asante kwa kujumuika pamoja nasi, Ni heshima yetu kuwa pamoja na wewe!

Wako katika utumishi,

*Timu ya Strategic Impact*

# "STRATEGIC IMPACT KUJIZIDISHA!"

Kauli hiyo inatangaza moyo wa harakati zetu. Tunafuata amri ya Yesu ya kuwafunza viongozi **wanaozidisha** wanaofanya wanafunzi **wanaojizidisha** na kuanza **kuzidisha** makanisa - ili kila mtu apate kusikia kuhusu tumaini pekee la uzima wa milele katika Yesu Kristo.

Mwongozo unaoshikilia mikononi mwako umeundwa ili **kukusaidia** kukufundisha na kukuwezesha kuwa mzidishaji. Unaposhiriki katika vipindi hivi, mwalimu wako atakutayarisha kuzidisha wanafunzi, viongozi, na hata makanisa. Lakini, huo ni mwanzo tu. Unapojifunza na kuishi mafunzo haya, **tunatamani uyatumie pia kuwafunza wengine kuzidisha.**

Utaona mwanzoni mwa kila kipindi kile kipindi hicho kimeundwa kufanya. Haya yamefafanuliwa katika malengo manne:

1. **Lengo** la jumla la kongamano: Dhumuni kuu la kongamano.
2. Nini cha **kujua**: Mafundisho au habari ambayo inapaswa kujifunza.
3. Jinsi mtu anapaswa **kujisikia**: Motisha au msukumo ambao washiriki wanapaswa kupokea kutokana na kipindi.
4. Nini cha **kufanya**: Muhimu zaidi, ni maombi gani au hatua gani washiriki wanapaswa kuchukua kama matokeo ya kikao.

Malengo haya manne kwa kila kipindi yameundwa kwa ajili ya wewe kuanza kujifunza na kuishi kutokana na mafunzo kutoka kwa kila kipindi. Malengo haya manne pia yamekusudiwa **kukusaidia kuzidisha** kwa kutumia malengo haya hayo ili kupitisha mafunzo haya kwa wengine. Ili kukusaidia kufanya hivyo, mambo yote makuu ya kufundishia na mambo madogo ya muhtasari yamejumuishwa kikamilifu.

Ombi letu ni kwamba uchukue na kutekeleza mafunzo haya katika maisha yako mwenyewe, na kisha uyatumie kuwafundisha wengine ili nao wajifunze, wayaishi, na kuyazidisha kwa kuwafundisha wengine kuzidisha hadi Agizo Kuu litimie.

Wako katika utumishi,

*Timu ya Strategic Impact*

# Strategic Impact Kujizidisha

*Viongozi ✣ Wanafunzi ✣ Makanisa ✣ Harakati*

## UTAMBULISHO:

**Sisi ni viongozi wenye mtazamo wa aina moja wa mtembeo, wenye mzigo na kujitoa kwa Yesu Kristo na kwa kila mmoja wetu ili kutimiza Agizo Kuu.**

## MAONO:

**Tupo ili kumpa kila mtu tumaini pekee la uzima wa milele katika Yesu Kristo katika maisha yetu, au kufa tukijaribu.**

*"Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari."* - Mathayo 28:18-20

## MALENGO:

Tunawafundisha viongozi watakaozidisha wanafunzi watakaowasha moto wamtembeo wa upandaji wa makanisa kila mahali.

*"...na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi hayo ukawakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine."* - 2 Timotheo 2:2

## MKAKATI:

Tunatengeneza timu za viongozi kimkakati kwenye miji ya ulimwengu ili kuzidisha mtembeo wa kupanda makanisa katikati ya kila kundi la watu.

*"(Paulo) akawatenga wanafunzi, akahojiana na watu kila siku katika darasa ya mtu mmoja, jina lake Tirano. Mambo haya yakaendelea kwa muda wa miaka miwili, hata wote waliokaa Asia walisikia neno la Bwana."* - Matendo 19:9-10

## MCHAKATO:

***Semina ya Maono* (VS)**
"Kuona Agizo Kuu."
*Utambulisho wa siku moja wa Strategic Impact.*

***Uzinduzi wa Wanafunzi Wanaojizidisha* (MDL)**
"Kupata Uzoefu wa Agizo Kuu."
*Maono ya mafunzo ya vitendo yakuwafanya wanafunzi wanaojizidisha.*

***Uzinduzi wa Kiongozi* (LL)**
"Kujifunza Agizo Kuu."
*Kupata uzoefu mkubwa wa kukua binafsi katika uongozi, na upandaji wa makanisa.*

***Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea* (SAFARI)**
"Kuliishi, Kuliongoza, na Kuzindua Agizo Kuu."
*Safari ya Maisha Kuufikia Ulimwengu Wako Ulipoptea kwa njia ya kuwafanya wanafunzi wanaojizidisha, makanisa, viongozi na mitembeo..*

***Mafunzo Mahususi ya Kiongozi* (LIT)**
"Kukua Katika Agizo Kuu."
*Kupata uzoefu mahususi kwa wale waliokwenye Safari ya kukua katika tabia ya uongozi na ubobezi wa uongozi kwa ajili ya Agizo Kuu.*

# Hatua 10 za Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea (v3.0)

## Hatua 1: Badili Kufikiri Kwako

*Badili Fikra toka hwenye malengo ya "kulijenga kanisa langu" waza "kuifikia jamii yako iliyopotea → nchi →dunia."*
*(Mathayo 28:18-20; Matendo 1:8; Matendo 20:24)*

## Hatua 2: Omba

*Ombea watenda kazi kwa ajili ya mavuno! (Luka 10:2; Matendo 13:1-3)*

## Hatua 3: Tangaza Maono

*Eleza Maono ya Mungu kwa watu wake juu ya kulifikia eneo lako kwa ajili ya kueneza Injili. (Matendo 1:8; 13:1-3)*

## Hatua 4: Kusanya na Uandae Timu

*Tambua, chagua, Kusanya na Uandae Timu ya angalau watu wawili wapanda makanisa kila mwaka. (Matendo 14:21-28; 19:9-10; Wakolosai 1:7; 2 Timotheo 2:2)*

## Hatua 5: Chagua Mahali

*Kwa njia ya maombi chagua mahali au kikundi cha watu wa Mungu ambao Mungu anakuongoza kuwafikia kwa Injili. (Matendo 16:6-40)*

A. *Tambua mahali ambapo Roho Mtakatifu anakuongoza kuanzisha kanisa la nyumbani..*
B. *Tafiti mahitaji yao, ngome zinazotawala, na shughuli za eneo hilo ambazo zinaweza kuathiri hilo kanisa jipya au uliyoanzisha.*

## Hatua 6: Fanya Unjilisti

*Wahubirie watu waliopo katika hilo eneo. (Matendo 5:42; 14:21,25; 20:20)*

## Hatua 7: Wafundishe Wanafunzi Wapya Walioamini

*Wafundishe waamini wapya mahali au katika eneo lao ulilowakuta.*
*(Matendo 14:22; 20:20)*

## Hatua 8: Wakusanye Waamini Wapya

*Kukusanya waumini wapya pamoja kwa vipaumbele vinne vya huduma ya kanisa:*

A. *Kuabudu (Matendo 2:42-43; 1 Corinthians 14:26-35; 16:1-2; Wakolosai 3:16),*
B. *Ukuaji (Matendo 2:42; Wakolosai 4:16; 2 Timotheo 4:2),*
C. *Ushirika (Matendo 2:44-46; 8:35-38; Waefeso 4:11-16),*
D. *Unjilisti (Matendo 2:47; 5:42; 8:4; 19:10; Wafilipi 2:15-16).*

## Hatua 9: Zidisha Wanafunzi

*Zidisha wanafunzi walio katika kanisa jipya kwa kurudia tena hatua hizo 8 za mwanzo. (1 Wathesalonike 1:7-8)*

## Hatua 10: Fungamanisha Mikono Pamoja ili Kuzindua Mtembeo

*Fungamanisha mikono na viongozi wengine kuzindua mtembeo wa kuzidisha wanafunzi ili kutimiza Agizo Kuu.*

***www.StrategicImpactInternational.com***

STRATEGIC IMPACT INTERNATIONAL

# *UZINDUZI WA KIONGOZI* ©

## *KATABU CHA MWALIMU*

## *"KUPATA UZOEFU WA AGIZO KUU"*

# *MWONGOZO WA VIPINDI*

## *Strategic Impact - Uzinduzi wa Kiongozi*
## Kipindi 1: *Sisi Ni Nani na Kwa Nini Tupo Hapa?*

**MAELEZO KWA UFUPI:**

**Lengo**: Mnenaji ataeleza moyo wa *Strategic Impact* na kutoa maelezo kwa ufupi kuhusu *Uzinduzi wa Kiongozi*.

**Kujua**: Viongozi wataelewa ni kitu gani ambacho *Strategic Impact* itafanya na yale ambayo hatuwezi kufanya wakati wa *Uzinduzi wa Kiongozi*.

**Kujisikia**: Viongozi watatiwa moyo kwa mafunzo na zana ambazo watapewa kwa ajili ya huduma zao.

**Mambo ya Kufanya**: Viongozi watajitoa na kushiriki maeneo yote ya *Uzinduzi wa Kiongozi*.

**Utangulizi:**

- Maelezo ya awali ya *Strategic Impact* — Tunatoa mafunzo kwa viongozi watakaowaandaa wanafunzi wanaojizidisha ambao wataanzisha mtembeo wa upandaji makanisa ili kutimiza Agizo Kuu.
- Toa ushuhuda wa mambo ambayo Mungu anafanya sasa kupitia *Strategic Impact* katika maeneo mbalimbali.

**SISI NI NANI:** Sisi ni viongozi wenye mtazamo wa aina moja wa **mtembeo**, wenye mzigo na kujitoa kwa Yesu Kristo na kwa kila mmoja wetu ili kutimiza Agizo Kuu.

1. **MAONO YETU:** Tunaishi ili kumpa kila mtu tumaini pekee la uzima wa milele ndani ya Yesu Kristo.
   *"Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari."* (Mathayo 28:18-20)

2. **MISHENI:** Tunawafundisha viongozi watakaozidisha wanafunzi watakaowasha moto wamtembeo wa upandaji wa makanisa kila mahali.
   *"...na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi hayo ukawakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine."* (2 Timotheo 2:2)

3. **MKAKATI:** Tunatengeneza timu za viongozi kimkakati kwenye miji ya ulimwengu ili kuzidisha mtembeo wa kupanda makanisa katikati ya kila kundi la watu.
   "*(Paulo) akawatenga wanafunzi, akahojiana na watu kila siku katika darasa ya mtu mmoja, jina lake Tirano. Mambo haya yakaendelea kwa muda wa miaka miwili, hata wote waliokaa Asia walisikia neno la Bwana.*" (Matendo 19:9-10)

4. **MCHAKATO:**
   ***Semina ya Maono*** **(VS)** — "Kuona Agizo Kuu."
   Utambulisho wa siku moja wa *Strategic Impact*.

   ***Uzinduzi wa Wanafunzi Wanaojizidisha*** **(MDL)** — "Kupata Uzoefu wa Agizo Kuu."
   Maono ya mafunzo ya vitendo yakuwafanya wanafunzi wanaojizidisha.

   ***Uzinduzi wa Kiongozi*** **(LL)** — "Kujifunza Agizo Kuu."
   Kupata uzoefu mkubwa wa kukua binafsi
   katika uongozi, na upandaji wa makanisa. Haya ndiyo tutafanya katika siku hizi ambazo tutakuwa pamoja.
   ***Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea*** **(*Safari*)** — "Kuliishi, Kuliongoza, na

Kuzindua Agizo Kuu."

*Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea* kwa njia ya kuwafanya wanafunzi wanaojizidisha, makanisa, viongozi na mitembeo. We hope that each of you will start the *Safari* at the end of this *Uzinduzi wa Kiongozi*.

***Mafunzo Mahususi ya Kiongozi* (LIT)** — "Kukua Katika Agizo Kuu."

Kupata uzoefu mahususi kwa wale waliokwenye *Safari* ya kukua katika tabia ya uongozi na ubobezi wa uongozi kwa ajili ya Agizo Kuu.

**MAMBO AMBAYO *STRATEGIC IMPACT* HAIWEZI KUFANYA:**

1. *Strategic Impact* **HATUTOI pesa** kwa wachungaji/viongozi au kuomba pesa kutoka kwako.

2. *Strategic Impact* **HATUJENGI** kanisa la mtu yeyote.

3. *Strategic Impact* **HAITAKUWA** bwana kwa mtumishi yeyote na kuonekana kama tuna **majibu** ya maswali yote.

4. *Strategic Impact* **HAITAKUAMULIA mafundisho** ya kufuata.

5. *Strategic Impact* **HATUTAPANDA** makanisa yatakayoitwa "*Strategic Impact*"… Tupo hapa kukusaidia WEWE NA KANISA lako kupanda makanisa.

6. *Strategic Impact* **HATUTAFANYA kazi yako**:
   Tutakapoenda mbinguni, Mungu hataniuliza **mimi**, "kwamba kwa nini hujafika , ___*(taja nchiau eneo ulilopo)*___ kwa injili ya Yesu Kristo?" Badala yake utaulizwa **wewe**.

**KWA NINI TUPO HAPA — Tupo Hapa Leo Ili Kutimiza Mambo 6:**

1. **Kukua katika uhusiano wetu na Kristo.** (2 Petro 3:18)
   - Hili ni jambo muhimu sana kwa kila mmoja wetu. Huu ndio msingi wa kila kitu tunacho kifanya katika maisha na huduma.

2. **Kujifunza Mikakati ya *Hatua 10* (*Hatua 10 za Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea*) za kuzidisha wanafunzi watakaopanda makanisa ili kufikia nchi (maeneo yao) na ulimwengu.**
   - Shabaha yetu siyo kuanzisha makanisa ya *Strategic Impact* bali ni kukusaidia wewe kuanzisha makanisa yatakayojizidisha.
   - Tutakuwa tukifanya uinjilisti pamoja katika jamii iliyotuzunguka kwa lengo la kuwafanya wengine kuwa wanafunzi watakaozidisha makanisa mapya!
   - Hatutafanya kazi yako, bali tutatembea pamoja na wewe na kuwafundisha watu wako kufanya uinjilisti kwenye jamii yako kwa lengo la kuwafanya wanafunzi wanaojizidisha ili kupanda makanisa.

3. **Kukupa wewe zana za kazi na uzoefu utakaokusaidia kuzidisha huduma yako.**
   - Utafundishwa na kushiriki katika kufanya uinjilisti wa mtu mmoja mmoja na kuwafundisha waongofu wapya ili uzidi kutembea kwenye maeneo haya ya kujizidisha ili yawe sehemu ya huduma yako — na ujiandae kuwafundisha wengine ili kufanya hivyo hivyo.

4. **Ili kupata ujuzi wa uongozi.**
   - Kilio cha kanisa ulimwenguni kote ni hitaji la viongozi wazoefu na wenye hofu ya Mungu! Ndiyo maana tumekualika kwenye *Uzinduzi wa Kiongozi*.

5. **Kupata marafiki katika maisha na huduma.**
   - Tunahitajiana. Hatuwezi kufanya kazi pekee yetu. Mungu ametuita tufanye kazi yake pamoja katika ulimwengu huu.

6. **Kuzindua mwanzo wa wewe na wengine kuanza timu ya *Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea*.**
   - *Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea* ina uwezo wa kufundisha maelfu ya viongozi wanaojizidisha, wanafunzi wanaojizidisha, wapanda makanisa wanaojizidisha, makanisa yanayojizidisha ili kutimiza Agizo Kuu.

**Tuko hapa kwa kuwa hizi ndizo siku njema za kuwa hai kama Wakristo ili kulitumikia shauri la Mungu!**

**Ni LAZIMA tuitumie kila fursa aliyotupa Mungu ili kutimiza makusudi yake kwa ajili yetu! (Waefeso 5:15-17)**

**NOTE**: Waombe viongozi mwombe pamoja kwenye *Uzinduzi wa Kiongozi*.

*STRATEGIC IMPACT - UZINDUZI WA KIONGOZI*

**KIPINDI 2: *KUELEWA MAONO YA MUNGU — HAKUNA KIKOMO***

**MAELEZO KWA UFUPI:**

**Lengo**: Mwalimu atawasilisha mwito mkuu wa Yesu wa uinjilishaji wa ulimwengu na utoaji Wake wa yote tunayohitaji ili kutimiza Agizo Kuu.

**Kujua**: Viongozi wataelewa kipaumbele cha Mungu na utoaji kwao katika wito Wake.

**Kujisikia**: Viongozi watakuwa na shauku ya kujitoa kikamilifu katika uinjilishaji wa ulimwengu.

**Mambo ya Kufanya**: Viongozi watajitolea kujisalimisha na kufanya kipaumbele cha Mungu kuwa kipaumbele chao wenyewe — na kuamini kwamba Yesu tayari ametoa yote ambayo ni muhimu ili kutimiza Agizo Kuu.

**MUHTASARI:**

**Utangulizi:**

- Kabla hatujajadili mchakato wa Kibiblia wa *HATUA 10 ZA KUUFIKIA ULIMWENGU ULIOPOTEA*, kabla ya kujizoeza juu ya kanuni za uongozi, kabla hatujajadili tabia ya Kimungu na utakatifu - kabla hata hatujazungumza kuhusu kiini cha Injili au ufuasi... kuna kitu cha msingi unachohitaji. kujua, kuelewa na kukumbatia kikamilifu. Hizi ndizo kanuni za msingi ambazo kila kitu kingine katika *STRATEGIC IMPACT* huchota maisha.
- Kwa hakika, usipokubali ukweli huu, mengine yale tunayokupa yatakuwa na maana kidogo, yatazaa matunda madogo, na hutakuwa na nguvu ndani yake.

**1. HAKUNA KIKOMO!**

A. **HAKUNA KIKOMO** kwa kile ambacho **Mungu** anaweza kufanya!

B. **HAKUNA KIKOMO** kwa kile ambacho Mungu anaweza kufanya **kupitia wewe**!

C. **HAKUNA KIKOMO** kwa kile ambacho Mungu anaweza kufanya kupitia wewe **unapojitoa kwa uwezo** wa **Mungu Roho Mtakatifu akaaye ndani yako**!

D. **Kuelewa** na **KUAMINI** kweli hizi ni muhimu kabisa katika kutimiza wito wa Mungu kwa kanisa kutimiza Agizo Kuu.

**2. Ujumbe wa mwisho wa Yesu na kipaumbele kwa wanafunzi Wake:**

A. Muda mfupi kabla ya Kristo kurudi Mbinguni, Aliwaagiza wanafunzi Wake wakutane naye kwenye Mlima wa Mizeituni. **Wanafunzi** walikuwa na matumaini kwamba angewapindua Warumi na mara moja ataweka Kiti cha Enzi cha Kimasihi duniani (Matendo 1:6), lakini **Yesu** alikuwa na ujumbe tofauti na kipaumbele cha kuwapa:

1. *"Akawaambia, Si kazi yenu kujua nyakati wala majira, Baba aliyoyaweka katika mamlaka yake mwenyewe"* (Matendo 1:7).

2. Badala ya mahangaiko yao, Yesu alitaka wajue jambo lingine ambalo lilikuwa muhimu zaidi: *"Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi"* (Matendo 1:8).

B. Kwa ahadi hii ya **Uwepo** Na **Nguvu** Zake, Yesu alizindua upanuzi wa kimataifa wa Kanisa Lake.

**3. Ujumbe sawa na kipaumbele ni kwa ajili YETU!**

A. Wewe na mimi ni wapokeaji wa **wito huu kutoka kwa Yesu**! Mungu anataka kutumia **maisha yako** kuleta ujumbe wa wokovu wa Kristo **kila mtu aliye hai duniani leo**!

B. **Hakuna wito mkuu**! **Hakuna misheni ya juu zaidi**!

C. Mungu ana kusudi: **"uinjilisti wa ulimwengu"** — Na Mungu anataka kukutumia **WEWE** kutimiza kusudi hilo!

D. Mungu anataka kutumia **MAISHA YAKO** kumpa **kila mtu aliye hai** duniani leo fursa ya kusema "**Ndiyo**" kwa Yesu!!

**4. Tayari una kila kitu unachohitaji ili kutimiza wito huu wa Mungu!**

A. Hii ndiyo sehemu ya kutia moyo: Mungu tayari ametoa **kila rasilimali unayohitaji** ili kufikia ulimwengu kwa ajili ya Kristo!

B. **NISIKIE**: **Tunapowasilisha** maisha yetu kwa makusudi ya Mungu, **HAKUNA KIKOMO** kwa kile Anachoweza kufanya kupitia!

1. Kufikia watu bilioni 8 inaonekana kama kazi "isiyowezekana," lakini kwa kweli, si vigumu zaidi kwa Mungu kufikia ulimwengu Wake kuliko ilivyo kwako au mimi kutembea kwenye chumba na kugeuza swichi ya taa.

C. Yeye ni Mungu — Na Amewekeza mamlaka **Yake** na **nguvu Zake** NDANI YETU ili kufanya **kazi Yake.**

**5. Maandiko yanayofunua moyo hasa wa Mungu:**

A. **Mungu anataka watu wote waokolewe**: *"Bwana… hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba"* (2 Petro 3:9b).

B. **Tayari tunazo rasilimali zote tunazohitaji ili kutimiza Agizo Kuu**: *"Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa…"* (2 Petro 1:3a)

C. **Hakuna sababu moja halali kwa nini hatuwezi kuweka Injili mikononi mwa kila mtu aliye juu ya uso wa dunia katika maisha yetu:** *"Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi…"* (Mathayo 28:18b-19a).

**Hitimisho:**

◉ Huu ndio **moyo** hasa **wa Mungu** — kuupa ulimwengu wake uliopotea tumaini pekee la uzima wa milele kwa njia ya imani katika Kristo!

◉ Tunakupa changamoto ya kujitolea leo - bila kuzuilia **CHOCHOTE** — kufikia kizazi chetu na Injili ya Yesu Kristo!

◉ Unapojitoa kwa ajili ya uinjilishaji wa ulimwengu, Mungu atasonga mbingu na dunia **kutumia maisha yako kutimiza Agizo Lake Kuu!**

**MAELEZO KWA UFUPI:**

**Lengo**: Mnenaji atatoa picha ya jumla ya namna mkakati wa *HATUA 10* unavyowezakusaidia kumfikia kila mtu kwenyemji, taifa, na kandakwa injili.

**Kujua**: Viongozi wataelewa umuhimu wa *HATUA 10 ZA KUFIKIA ULIMWENGU WAKO ULIOPOTEA*.

**Kujisikia**: Viongozi watajisikia mzigo na changamoto ya kuyafikia mataifa yao kwa ajili ya Kristo na kuwa na shauku ya kupata nyenzo kwa ajili ya kukamirisha hiyo kazi.

**Mambo ya Kufanya**: Viongozi watajifunza alama za *HATUA 10 ZA KUFIKIA ULIMWENGU WAKO ULIOPOTEA* na kuweza kuzisema *HATUA 10* kwa yeyote wakati wowote.

**SHAUKU YAMUNGU:**

6. **Je Mungu anataka nini?** (1 Timotheo 2:4). Mungu anataka kila mtu aokolewe na kupata maarifa ya kweli.

**MKAKATI WA MUNGU:**

7. **Mungu anatimizaje shauku yake?** (Mathayo 28:18-20; Matendo 1:8) Mungu anatimza shauku yake kupitia watu wake kanisa lake ambalo linatakiwa kuipeleka injili kwa kila mtu aliyeko kwenye hii Sayari. Mungu anataka kutenda kupitia wewe ndani ya kanisa lake katika karne ya 21 kama alivyofanya kwa njia ya kanisa lake katika karne ya 1.

8. **Mkakati wa Mungu ukoje?** (Matendo 19:8-10; 20:24; 2 Timotheo 2:2; Wakolosayo 1:7-8, 4:12) Tunauona kwenye kurasa za Agano Jipya:

**Maswali Ya Hiyari Kwa Washiriki** (Tumia maswali mengi kadri unavyopata muda. Wagawanye viongozi kwenye makundi ya watu 3- 5 kwa ajili ya majadiliano, kisha mwakilishi wa kila kundi ashirikishe kundi lote): Soma Matendo 19:8-10

- Paulo alikuwa anafanya nini? Alikuwa anafanyia wapi? Matokeo yake yalikuwa nini?
- Je, Kila mtu katika Bara la Asia alimwamini Yesu? Ni kitu gani ambacho kila mwanaume, Mwanamke, Mvulana, na msichana waliokaa Asia walikipata?
- Je, unadhani matokeo kama haya yaweza kutokea kwenye mji, Mkoa, na Taifa lako?
- Unadhani watu wote waliokuwa Asia walisikiaje Injili? Je, wote walikuja kumsikiliza Paulo kwenye ukumbi wa Tirano kule Efeso? Kama si hivyo ilikuaje basi? (tazama Wakolosai 1:7- 8; 4:12 – Mji ulioko Asia).

**9. Mkakati wa Mungu ndio njia pekee ya mji/kanda/ulimwengu kufikiwa na Injili kwa ukamilifu.**

A. Badili kufikiri kwako na ujitoe kwa ajili ya misheni ya Mungu ya kumshuhudia Yesu (Matendo 20:24)

B. Waandae wanafunzi watakaojizidisha. (Matendo 19:8-10; 2 Timotheo 2:2)

C. Wakusanye wanafunzi wanaojizidisha kwenye makanisa yanayoandaa wanafunzi (Matendo 2:42- 47; 14:21- 24)

D. Zidisha makanisa yanayoandaa wanafunzi ili yaenee ili kila mtu asikie namna ya kumjua Kristo. (Matendo 19:10; Wakolosai 1:7-8; 4:12)

**10. Jinsi gani tunaweza tukaufanya mfano huu wa Agano Jipya wakati wetu? Fuata *Hatua 10 za Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea* kwa Injili.**

A. Hizi *Hatua 10* siyo mpya. Ni hatua ambazo Mitume, wanafunzi, na makanisa ya Agano Jipya walitumia kuufikia ulimwengu wao.

B. Nitakueleza kuhusu *Hatua 10* na tutaenda kutazama kila Hatua kadri tunavyoendelea na kongamano. (Fungua ukurasa wa 7 kwa muhtasari wa *Hatua 10 za Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea*)

C. Hebu sasa tuangalie *Hatua 2* za mwanzo:

**_Strategic Impact - Uzinduzi wa Kiongozi_**
**Mkakati wa Kuufikia Ulimwengu Wako Ulipoptea**
**_Hatua 1_: Badili Kufikiri Kwako, _Hatua 2_: Omba**

**MAELEZO KWA UFUPI:**

**Lengo**: Mnenani ataeleza na kudhihirisha jinsi ya kubadili kufikili kunavyoanzisha kuufikia ulimwengu uliopotea na kwamba maombi ndiyo yanayosukuma matendo katika *Hatua zote 10.*

**Kujua**: Viongozi wataelewa *Hatua* 1, 2, na 3 katika *Hatua 10 za Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea*.

**Kujisikia**: Viongozi watajisikia changamoto kubadiri kufikiri kwao ili kujipanga na maono ya Mungu na kuomba kwa ajili ya mavuno kwa ajili ya Kristo katika Miji/Taifa.

**Mambo ya Kufanya**: Viongozi watajifunza alama za vidole za *Hatua 10 za Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea* na wataweza kuzisema *Hatua 10* kwa mtu yeyote na wakati wowote.

## Hatua 1: Badili Kufikiri Kwako

Badili Fikra toka hwenye malengo ya “kulijenga kanisa langu” waza “kuifikia jamii yako iliyopotea → nchi →dunia.”
(Mathayo 28:18-20; Matendo 1:8; Matendo 20:24)

A. Kristo hajakuita kujenga “kanisa kubwa” hiyo ni kazi yake! (Mathayo 16:18)

B. Kristo alikuita kuwafanya wanafunzi wanaojizidisha ambao wataufikia huu ulimwengu kwa injili. (Mathayo 28:18–20)

## Hatua 2: Omba

Ombea watenda kazi kwa ajili ya mavuno! (Luka 10:2; Matendo 13:1-3)

A. Ombea juu ya nani atakuwa kwenye timu yako na wapi utapanda kanisa jipya.

B. Omba kwa ajili ya watu watakao kuwa kwenye timu kwa ajili ya upandaji wa makanisa na mahali utakapo panda kanisa jipya wewe.

C. Orodhesha timu ya maombi watakao endelea kuombea mchakato huu kuanzia Mwanzo hadi mwisho.

D. Tunakutia moyo kuungana na mtembeo kwa Strategic Impact ulimwenguni kuomba kila siku saa 4:02 asubuhi kwa kufuata Luka 10:2; tukiomba kwa ajili ya watenda kazi ili kuleta mavuno ya kiroho kwa ajili ya Kristu.
   1. Tega kengele kwenye simu au saa yako ili kila siku saa 4:02 Asubuhi kukukumbusha kuomba.
   2. Kengele ikilia acha unachokifanya ili uombe
   3. Mwalike yeyote aliyekaribu na wewe ili muombe

## Hatua 3: Tangaza Maono

Eleza Maono ya Mungu kwa watu wake juu ya kulifikia eneo lako kwa ajili ya kueneza lnjili. (Matendo 1:8; 13:1-3)

A. Elezea wazi wazi namna ambavyo Mungu anataka kukutumia wewe na kanisalako kutimiza Agizo Kuu katika eneo lako.

B. Mara kwa mara kwa kutumia maneno yako “Chora picha” ya maono haya kwa watu wako.

C. Kueleza na kuyaishi maono ya Mungu kwa ajili ya Agizo Kuu ndio wajibu wa kiongozi wa Kiungu.

## KIPINDI 3: *MAONO YA KIONGOZI — KUUFIKIA ULIMWENGU ULIOPOTEA*

**MAELEZO KWA UFUPI:**

**Lengo**: Mnenaji ataeleza maana ya uongozi, ataonyesha umuhimu wa maono katika uongozi, atafundisha maono ya Mungu kuhusu Agizo Kuu na kuwatia moyo viongozi kumtafuta Mungu kwa sehemu yao katika maono ya Mungu makubwa kuhusu Agizo Kuu.

**Kujua**: Viongozi wataelewa kwamba maono ni picha ya Mungu ya wakati ujao na huduma yao katika mpango wa Agizo Kuu.

**Kujisikia**: Viongozi watajisikia kushawishika juu ya wito wa Mungu anaowaitia kuutekeleza.

**Mambo ya Kufanya**: Viongozi wataomba, wataandika na kukariri, maono ya Mungu kwa ajili ya maisha yao kulingana na mpango wa Agizo Kuu.

**Utangulizi:**

- Hitaji kubwa katika kanisa ni kupata viongozi wacha Mungu watakao lihamasisha kanisa kutimiza Agizo Kuu.

- Mungu anataka kukutumia wewe kuwashawishi **watu wake** kutimiza **makusudi yake**.

- Bila uelewa wa wazi kuhusu uongozi huwezi kuongoza vizuri, na bila kuelewa maono kama kiongozi huwezi kuongoza ili kutimiza lengo la Mungu kwa ajili yako na watu wako.

- Viongozi wengi wana maono ya mambo wanayotaka kutimiza. Lakini, kama viongozi wa kikristo tunahitaji maono ambayo yanakubaliana moja kwa moja na yale ambayo Mungu anataka tutimize kulingana na neno lilivyotamka yaani Biblia.

- Tunahitaji kuomba, kuiangalia Biblia, kuota, na kisha kufafanua wajibu wetu wa kipekee katika kutimiza maono ya Mungu kwa ajili ya KUUFIKIA ULIMWENGU ULIOPOTEA kwa kufuata **mpango na mtindo uliofunuliwa na Mungu.**

**UONGOZI**

1. **Kiongozi ni nani?** UFAFANUZI: Ni mtu anayewashawishi wengine.

   A. Mambo manne ya MSINGI YALIYOMO kwenye uongozi:
      1. **Maono**: Kujua unakokwenda.
      2. **Mkakati**: Kujua namna ya kufika unakokwenda.
      3. **Ushawishi**: Kuamsha shauku ya watu wengine kushiriki.
      4. Lakini katika uongozi wa kikristo kuna jambo la nne muhimu ambalo ni **Tabia**!
         **Tabia** ni **uadilifuuliyothibitishwa** kwa muda mrefu na kusababisha kuaminiwa.

2. **Nini maana ya Uongozi wa Kikristo?** UFAFANUZI: Ni kuwashawishi watu kutoka kwenye msingi wa tabia ya kiungu ili kutimiza **maono** ya kiungu.

**Maswali ya hiyari kwa washiriki** (Tumia maswali mengi kadri unavyopata muda. Wagawanye viongozi kwenye makundi ya watu 3- 5 kwa ajili ya majadiliano, kisha mwakilishi wa kila kundi ashirikishe kundi lote.)

Muombe mtu mmoja asome Ufunuo 7:9-10, kisha ULIZA:

- Yohana alikuwa wapi alipoona haya maono ya mbinguni? Kwa nini alikuwa huko? Wale Mitume wengine 11 waliotembea na Yohana na Yesu walikuwa wapi?
- Ni agizo gani ambalo Yohana wa wale Mitume 10 walipokea kutoka kwa Yesu kabla hajapaa kwenda mbinguni? Je walikuwa ni waaminifu kutiiAgizo hili? Je walifika katika kila taifa, kabila, watu na lugha?
- Yohana aliona nani wakimuabudu Yesu? Waabudu hawa wote walitoka wapi? Je Yohana aliona kitu chochote kilichotokea au ilikuwa nikwa wakati ujao?
- Mungu alimpa Yohana maono halisi ya wakati ujao. Haya maono yalimtia moyo Yohana kuendelea na kazi ambayo Yesu aliwapa — haikujalisha hali yake ilikuaje.

**MAONO — Ni Jambo Muhimu katika Uongozi**

1. **Maono ni nini?** UFAFANUZI: Maono ni uwezo wa "kuona" yale ambayo bado hayapo.

   A. Maoni ni "binamu" wa Imani kama ilivyoelezwa katika Waebrania 11:1.

2. **Kwa nini maono nimuhimu?**

   A. Maono ndiyo mwanzo wa uongozi. Kama hujui **unakokwenda** kuwezi kuandaa **mkakati** na pia huwezi kuwashawishi wengine kujiunga na wewe au kukufuata.

   B. Bila maono wewe na watu wako hamuendi kokote, "mtakuwa mnapiga kwata mahali pamoja." Kwa vile hamuendi kokote utakuwa unawachosha watu wako.

   C. Maono yanawaunganisha watu kwa kusudi la pamoja, na katika lengo la kiungu la kuhamasisha watu kutenda!

**MAONO YA MUNGU**

1. Kama Wakristo tunayafanya maono yetu **yaendane** na maono ya Mungu ya kutimiza Amri Kuu kupitia Agizo Kuu.

   A. Kwanza tunahitaji kuuliza **"Kitu gani ambacho ni muhimu sana kwa Mungu?"**

      1. Kutokana na upendo, Mungu kwa hiyari yake alimtoa mwanae wa pekee ili **kukomboa wanadamu** (Yohana 3:16).

      2. Kutokana na upendo, Mwana wa Mungu alikuja kutafuta na kuokoa waliopotea (Luka 19:10).

      3. Mungu anataka kila mtu asikie Injili na kuna siku jambo hili litatimizwa (Timotheo 2:4; 2 Petro 3:9; Mathayo 24:14; Ufunuo 7:9-12)

      4. Mungu hataki mtu yeyote asiangamie, hata hivyo wale wanaokufa bila Kristo hupita milele kutoka kwa rehema ya milele. (Mathayo 13:49-50; Waebrania 9:27)

      5. Kutimiza Agizo Kuundo njia bora ya kutimiza Amri Kuu (Mathayo 22:36-40; 2 Wakorintho 5:14).

B. Hii mistari inatuonyesha **kipaumbele cha maono** ya Mungu ni kutimiza Amri Kuu kwa kutimiza Agizo Kuu.

1. Ni lazima tufungue "Macho yetu **KUONA** kila mtu katika miji yetu, Taifa na ulimwengu ili waupate upendo wa Mungu kwa njia ya kusikia Injili"

2. Mungu ametupatia **kila kitu** tunachokihitaji ili kukamilisha hili kupitia nguvu na nafsi ya Kristo (2 Petro 1:3).

C. Hatuhitaji maono **MAPYA**! Tunahitaji tu kuelewa na kujitoa kwa ajili ya maono HALISI kwa ajili ya Kanisa lake - kisha kwa njia ya maombi tugundue **WAJIBU WETU** katika kutimiza maono ya Mungu!

1. Maono ya Mungu siyo ndoto **yako** ya mafanikio ya Duniani (Wakolosai 3:2)!

2. Maono ya Mungu kwa ajili yako ni vile atakavyokutumia wewe kutimiza makusudi **YAKE** (Jeremia 1:5).

**WAJIBU WAKO KATIKA MAONO YA MUNGU**

1. Wewe na watu wako **munawajibu maalumu** wa kutimiza maono ya Mungu. Wewe na watu wako muna **mchango** wa **kipekee** kuyafanya makusudi yake ya milele Wewe na watu wako muna **hatima ya kiungu** mnayotakiwa kuitimiza!

A. Ili kutimiza hili kwanza anza na maisha yako mwenyewe…

1. **Gundua** hatima yako katika kuwafanya mataifa kuwa wanafunzi (Mathayo 28:18 – 20).

2. **Endeleza** hatima yako — endeleza vipawa vya kipekee na ujuzi aliokupa wewe na watu wako. (2 Petro 1:5; 2 Wakorintho 9:8; Waebrania 10:24).

3. **Timiza** hatima yako kwa kutimiza wito wa Mungu kwenye maisha yako (Matendo 20:24; 2 Timotheo 4:7).

B. Ili kukamilisha hili jambo la pili ni lazima — Upandikize maono kwa watu unaowaongoza. Kwa namna gani?

1. Yadhihirishe maono kwa watu wako kupitia mfano wa maisha yako, iishi NDOTO ya Mungu!
   a) Uwe mfano wa matendo wa namna ya kutimiza maono ya Mungu.
   b) Toa muda wako, uangalifu na juhudi katika kupeleka Injili kwa watu waliopotea katika eneo lako.
   c) Waonyeshe watu wako kipaumbele cha Amri Kuu na Agizo Kuu kupitia maisha yako.

2. "Chora picha" kwa njia ya maneno yako ya wakati ujao ambavyo itakuwa halisi na wazi wazi — ili wengine waweze **kuiona**!
   a) Itaonekanaje kuhubiri kwa jirani zako, mji wako, wilaya, mkoa na Taifa lote?
   b) Ni nafasi gani munayotumika wewe na kanisa lako katika kuwafikia waliopotea?

3. Palilia na tunza pendo lako binafsi la kutimiza maono ya Mungu ya kuufikia ulimwengu kwa Injili.
   a) Ni jinsi gani unaweza ukayafanya haya maono yawe moto kwenye moyo wako mwenyewe?

b) Ni jinsi gani unaweza ukayafanya haya maono kuwa moto kwenye mioyo ya watu wako?
  - Katika hali endelevu pitia kwenye Biblia uone maono ya Mungu kwa ulimwengu
  - Mara kwa mara ombea juu ya kuwafikia waliopotea kwa Injili katika eneo lako.
  - Shirikiana na viongozi wenye mzigo kwa ajili ya maono ya Mungu
  - Tenga muda wa kupata ndoto na kutambua wazi wazi wajibu wako katika kutimiza maono ya Mungu.
  - Chukua hatua mara kwa mara ya kuwashirikisha Injili waliopotea.

**MAMBO YA KUFANYA:**
Chukua muda wa peke yako sasa kuomba na kufanya mambo yafuatayo:
1. JIBU: Unaweza ukayaelezaje maono ya Mungu kwenye maisha yako katika kutimiza Agizo Kuu?

2. Andika "andishi la kwanza" liwe wazi wazi, na lenye kukumbukwa, kuhusu maono ya Mungu juu ya maisha yako na huduma katika **sentensi moja**.

*Strategic Impact - Uzinduzi wa Kiongozi*
**Mkakati wa Kuufikia Ulimwengu Wako Ulipoptea**
***Hatua 4*: Kusanya na Uandae Timu, *Hatua 5*: Chagua Mahali , *Hatua 6*: Fanya Unhilisti**

**MAELEZO KWA UFUPI:**

**Lengo**: Mnenaji atapitia *Hatua 10 za Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea* Ana kuelezea wazi wazi *Hatua* 4, 5, na 6.

**Kujua**: Viongozi wataelewa *Hatua* 4, 5, na 6 katika *Hatua 10 za Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea*.

**Kujisikia**: Viongozi watajisikia hamasa na changamoto binafsi kutambua na kuandaa timu, kuchagua eneo na kuwahubiria watu wa eneo hilo.

**Mambo ya Kufanya**: Viongozi watajifunza alama za mikono za *Hatua 10 za Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea* kuweza kusema *Hatua 10* kwa mtu yeyote wakati wowote.

**Utangulizi:**

- Pitia *Hatua 3* za mwanzo na alama za mikono. *Hatua 1*: "Badili kufikiri kwako," *Hatua 2*: "Omba," na *Hatua 3*: "Tangaza Maono."
- Waelekeze viongozi warudie kutaja hatua hizo baada yako kwa kuonyesha alama za mkono kwa kila hatua.

## Hatua 4: Kusanya na Uandae Timu

Tambua, chagua, Kusanya na Uandae Timu ya angalau watu wawili wapanda makanisa kila mwaka.
(Matendo 14:21-28; 19:9-10; Wakolosai 1:7; 2 Timotheo 2:2)

A. Mwombe Mungu akuonyeshe nani uwaandae Kama timu ya wapanda makanisa.

B. Tumia muda wa kutosha kuiandaa hii timu katika mahusiano yao binafsi na Kristo na uwaongoze kwenye mchakato wa kupanda kanisa jipya.

Ili kuiandaa hii timu unahitaji **mkakati** na **zana** ya kufundishia.

The *Strategic Impact* ***Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea*** ni Zana unayoweza kutumia kufundisha Timu yakokufanya uinjilisti, kuandaa wanafunzi, kupanda makanisa mapya na kuzidisha viongozi wapya (kama ilivyoelezwa hapa chini).

- Tumeitwa kufanya sehemu yetu ili kutimiza maono ya Mungu ya Agizo Kuu.

- Swali la kujiuliza ni hili, "Ni jinsi gani tutampa fursa kila mtu kwenye miji yetu, mikoa yetu, nchi zetu kanda zetu kusema 'Ndiyo' kwa Yesu — ambaye ndiye tumaini pekee la uzima wa milele?"

- Viongozi wa Agano Jipya wanadhihirisha mkakati wa kujizidisha ili kuyafikia maeneo kwa Injili.

**KUJIZIDISHA HADI KIZAZI CHA 4**

1. Paulo **aliwafundisha** wanafunzi katika mji mmoja (Efeso) na akalifikia taifa lote (Asia) kwa Injili kwa muda wa miaka miwili! Omba mtu mmoja asome Matendo 19:9-10.

2. Paulo alifuata mfano wa 2 Timothy 2:2: alifundisha wakufunzi **wanaojizidisha**, waliofanya wanafunzi **wanaojizidisha** walioanzisha makanisa **yanayojizidisha**. Huu ni mfano wa wanafunzi na makanisa ya Kolosai na Laudikia yaliyokuwa kwenye miji ya bara la Asia.
   A. **Paulo[1]** (mmoja wa wanafunzi) alimwongoza —> **Epafra[2]** katika Imani kwa Yesu (kule Efeso?), na kisha alifanya uinjilisti kwa watu wa Kolosai, (Wakolosai 1:5-8)

   B. **Epafra[2]** aliwafundisha —> **Arkipo[3]** na **Afia[3]** ambao walikuwa wanajishughurisha na kanisa la nyumbani kule Kolosai (Wakolosai 4:17; Filemoni 1:2)

   C. **Arkipo[3]** and **Afia[3]** ndiyo waliomfundisha —> **Nimfa[4]** ambaye alikuwa na kanisa karibu na Laodikia (Wakolosai 4:15)

   Katika mchakato huu tunaona vizazi 4: **Paulo[1]** (Efeso), **Epafra[2]** (Kolosai), **Arkipo[3]** na **Afia[3]** (Kolosai), **Nimfa[4]** (Laodikia).

**MKAKATI WA AGANO JIPYA**

3. Lazima **tufuate mfano** huu kama tunataka kuona matokeo kwenye miji yetu, nchi na kanda nzima!

   A. Mkakati wa msingi wa Agano Jipya: Uinjilisti, kuandaa wanafunzi, kupanda makanisa, mafunzo, kujizidisha (MCHAKATO HUU UNAJIRUDIA)!

      1. Mitume na waamini wengine walienda kwenye maeneo mapya, wakafanya uinjilisti na **kuwaleta watu kwenye Imani kwa Kristo**. (Mtendo 8:4-5; 11:19-21; 14:7; Wakolosai 1:8-10)
      2. Kisha **waliwafundisha waumini wapya** ili kuwasaidia kukua na kuzidisha wanafunzi. (Mtendo 14:21-22; 2 Timotheo 2:2)
      3. **Waliwakusanya waumini wapya kwenye kanisa jipya** (walikutana kwenye nyumba). (Mtendo 20:20; Warumi 16:6; 1 Wakorintho 16:19; Wakolosai 4:15; Filimon 1:2)
         a. makanisa hayakuwa na majengo, wala ratiba wala watumishi waliosimikwa.
         b. UFAFANUZI: **Kanisa** — Kanisa ni kusanyiko la wafuasi wa Yesu wanaoongozwa na viongozi wa kiroho wenye sifa, chini ya mamlaka ya Biblia wanaokusanyika mara kwa mara ili kumuabudu Mungu, kukua kiroho, kupendana na kuhudumiana na kwenda kuwafanya mataifa kuwa wanafunzi katika ulimwengu uliopotea.
         c. Wanafunzi walifanya kazi kama kanisa, kisha wakatawanyika ili kuwafanya wengine kuwa wanafunzi na kupanda makanisa mapya (Mtendo 2:42-27; 5:42).
      4. **Walichagua na kuwafundisha viongozi** ili kuongoza makanisa mapya (Prisila na Aqula, Arkipo, Nimfa), (Mtendo 14:23; 1 Wakorintho 16:19; Wakolosai 4:15; Filimon 1:2).
      5. **Wanafunzi na viongozi walipojizidisha** makanisa mengi Zaidi yalipandwa na kujizidisha mpaka miji yote, ikafikiwa na Injili.

**ZANA za *STRATEGIC IMPACT***

4. ZANA za *Strategic Impact* itakayokusaidia kufundisha timu yako kuwafanya wanafunzi wanaojizidisha na kupanda makanisa mapya inaitwa *"Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea"* (*Safari*)

   A. *Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea* ina hatua 5 kufikia vituo 5.
      1. *Hatua 1* — Wafanye **wanafunzi** waliokuwa na **kujizidisha**.
      2. *Hatua 2* — Panda **makanisa yanayojizidisha**.
      3. *Hatua 3* — Fundisha **viongozi wanaojizidisha**.
      4. *Hatua 4* — Zindua **mitembeo inayojizidisha**.
      5. *Hatua 5* — Andaa wafanya **mitembeo inayojizidisha**.

B. Mwisho wa *Uzinduzi wa Kiongozi*, tutakuomba ukusanye na kuandaa timu ya watu 3 - 5 ili kuanza mchakato wa kuanza *Safari*.
   1. Tutaeleza jinsi *Safari* inavyofanya kazi na namna ya kutumia Zana.
   2. Tutakupa zana zinazohitajika ili uendelee kuandaa na kufundisha timu hadi Kizazi cha 4.
   3. Tunawaombea kwamba wewe na timu yako mtajitoa kuanza mafunzo ya *Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea*.

## Hatua 5: Chagua Mahali

Kwa njia ya maombi chagua mahali au kikundi cha watu wa Mungu ambao Mungu anakuongoza kuwafikia kwa Injili. (Matendo 16:6-40)

A. Tambua mahali ambapo Roho Mtakatifu anakuongoza kuanzisha kanisa la nyumbani..

B. Tafiti mahitaji yao, ngome zinazotawala, na shughuli za eneo hilo ambazo zinaweza kuathiri hilo kanisa jipya au uliyoanzisha.

A. Katika hali ya maombi pambanua wapi Roho Mtakatifu anakuongoza kupanda kanisa jipya.
   1. Inaweza ikawa ni eneo la kijiografia mahali ambapo hapana kanisa linalowafanya watu kuwa wanafunzi.
   2. Inaweza ikawa kundi maalumu la watu mahali ambapo hapana kanisa linalowafanya watu kuwa wanafunzi.

B. Chunguza mahitaji, ngome na shughuri zinazoendelea kwenye eneo zinazoweza kuathiri kanisa jipya.

## Hatua 6: Fanya Unjilisti

Wahubirie watu waliopo katika hilo eneo. (Matendo 5:42; 14:21,25; 20:20)

A. Wafundishe timu yako kuwashirikisha wengine injili kwa urahisi na ufanisi katika eneo ambalo umelichagua.
   1. Lengo ni kuwapata na kuwafanya wanafunzi wanaojizidisha na kisha kuwakusanya kwenye kanisa jipya.
   2. Kupanda kanisa bila kufanya uinjilisti ni zoezi tu la kuwahamisha Wakristo toka kanisa moja kwenda kanisa jingine.

B. Wafuate watu mahali walipo ili uwashirikishe Injili (Mtaani, nyumbani, sokoni na makundi mbalimbali). Usitarajie watu kuja kwako!

Sasa tunaenda kukutambulisha kwenye *Mishale 3 Zana ya Tumaini na Maisha ya SI* ambacho Mungu amekitumia duniani kote ili kuwasaidia watu kuja kwenye imani kwa njia ya Yesu Kristo.

## KIPINDI 4: *ASILI YA INJILI: MAFUNZO YA UINJILISTI*

**MAELEZO KWA UFUPI:**

**Lengo**: Mnenaji ataelezea ujumbe wa injili kwa urahisi na kwa uwazi na kuwafundisha wahudhuriaji jinsi ya kushirikisha injili kwa kutumia *MISHALE 3 ZANA YA TUMAINI NA MAISHA YA SI*.

**Kujua**: Viongozi wataelewe asili ya ujumbe wa Injili.

**Kujisikia**: Viongozi wajisikie ujasiri kwamba wanaweza kushirikisha kwa uwazi na rahisi Injili na namna ya kutumia *MISHALE 3 ZANA YA TUMAINI NA MAISHA YA SI* baada ya kujifunza.

**Mambo ya Kufanya:** Viongozi wawe na uhakika wa uhusiano wao na Kristo na kushirikisha wengine Injili **(1)** wakati wae *UZINDUZI WA KIONGOZI* na **(2)** baada ya *UZINDUZI WA KIONGOZI* iwe ni mtindo wa maisha kutumia *MISHALE 3 ZANA YA TUMAINI NA MAISHA YA SI*.

**Utangulizi:**

◉ Kila kitu tunachokifanya katika mikutano ya *STRATEGIC IMPACT* lazima kihusishe Uinjilisti — kwa kuipeleka injili/habari njema ya Yesu Kristo kwa ulimwengu uliopotea.

◉ Lengo letu siyo kuwa na tukio la mafunzo tu bali ni wewe na wengine muliopitia mafunzo mshiriki katika kufanya uinjilisti kama sehemu ya maisha. **Hatufanyi** mafunzo bila kuhusisha. **Uinjilisti wa mtu mmoja mmoja.**

◉ Mara nyingi tumeshangazwa kwamba Wakristo hata wachungaji na viongozi — Wanashindwa kuelewa **asili** ya ujumbe wa Injili na **namna** ya kuushirikisha kwa wengine ili nao wapate uzima wa milele ndani ya Kristo.

◉ Kwa hiyo leo tungependa kupitia kwa **usahihi** ujumbe wa Injili **rahisi** na kisha kukupatia zana itakayokusaidia kuwashirikisha wengine.

◉ Kisha tutaenda huko NJE pamoja ili kuwashirikisha wengine Injili.

**ASILI YA INJILI**

1. **Asili ya injili ni KUAMINI KIFO cha kidhabihu, kuzikwa kwa mwili, na KUFUFUKA kwa Yesu Kristo. (1 Wakorintho 15:1-4)**
   A. Paulo anafafanua ujumbe wa msingi wa injili ambao aliwashirikisha watu waliopotea:
      1. Yesu Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu.

      2. Mwili wake ulizikwa.

      3. Alifufuka kutoka kwa wafu siku ya tatu.

      4. Wale watakaomwamini Yesu Kristo kama Mwokozi wao watasamehewa dhambi zao na kupokea uzima wa milele. (1 Wakorintho 15:1-2, 51-53)

   B. Tuwe waangalifu **tusiwachanganye** watu kuhusu wanachotakiwa kuamini ili kuokoka!
      1. Kuna mkanganyiko fulani kwenye ujumbe wa injili, unachanganywa na kazi, miujiza, uponyaji, kukemea mapepo n.k.

2. Kama matokea tumeona baadhi ya wachungaji na viongozi ambao hawana uhakika juu ya uhusiano wao na Mungu! Ikiwa hii inawakilisha wewe, au ikiwa hauna uhakika, tafadhali zungumza na mmoja wetu!

**2. Ni lazima tuwafunulie watu MAENEOMUHIMU ya injili na kuwapa fulsa iliyowazi kuitika na kumpokea Yesu kwa imani kama njia pekee ya kupokea uzima wa milele.**

A. Maeneo muhimu ya Ujumbe wa Injili:

1. Upendo wa Mungu kwa watu ulimwenguni. (Yohana 3:16)

2. Dhambi yetu na malipo yake ya kifo. (Warumi 3:23, 6:23)

3. Kifo cha Yesu Kristo, maziko yake, na kufufuka kwake — ndiyo njia pekee ya kumuendea Mungu. (Yohana 14:6; Warumi 5:8; 1 Wakorintho 5:3-8; 1 Timotheo 2:5; 1 Yohana 5:11-12)

4. Wokovu wa Mungu umetolewa kama zawadi kwa neema kwa njia ya kumuamini. (Yohana 1:12; Warumi 10:9-10; Waefeso 2:8-9)

B. Paulo mwenyewe aliomba maombi kwamba apewe fulsa ya kuhubiri injili na kuifafanua wazi wazi kwa wanaoisikia. (Waefeso 6:19-20; Wakolosai 4:3-4)

C. Nasi pia tuchukue **kila fulsa** kuhuburi injili rahisi kwa wengi kadri inavyowezekana!

**NYENZO RAHISI YA KUWASHIRIKISHA WENGINE ASILI YA INJILI**

**3. *Mishale 3 Zana ya Tumaini na Maisha ya SI* imetengenezwa ili kusaidia kuwashirikisha wengine ujumbe wa injili kwa urahisi na kuwapa fulsa ya kumpokea Yesu kwa imani.**

A. Nitakuonyesha namna ya kutumia nyenzo hii kuwasilisha Injili.

1. ** Onyesha matumizi ya *Zana*. Mwite mtu atakayejitolea ili uonyeshe mfano wa kumhubiri mtu mwingine Injili.

2. ** Fafanua maelezo ya namna ya kutumia *Zana*. Unapotoa maelezo onyesha hizo picha kwa viongozi.

B. <u>**MUHIMU**</u>: Baada ya maelezo toa fulsa kwa kila mtu kwenye *Uzinduzi wa Kiongozi* ili ambaye hajaokoka ampokee Yesu.

**JUMAPILI YA "INJILI":**

**4. Jumapili IJAYO kanisani kwako ifanye kuwa "jumapili ya injili."**

**MCHUNGAJI**: Toa **ushuhudawako** wa namna ambavyo ulimpokea Kristo.

**MCHUNGAJI**: Washirikishe wengine **ujumbe wa Injili kwa urahisi.**

**MCHUNGAJI**: Wape watu **fursa** ya **kumpokea Yesu Kristo kwa Imani** wakati wa ibada.

***Strategic Impact - Uzinduzi wa Kiongozi***

## Zana: *Jinsi Ya kutumia Mishale 3 Zana ya Tumaini na Maisha ya SI*

1. Mfahamu mtu unayetaka kumshirikisha naye kwa kuuliza kuhusu **HADITHI YAO**:
   - Jua kuhusu malezi yao ya kiroho
   - Uliza ikiwa mambo ya kiroho ni muhimu kwao.
   - Uliza ikiwa wanahisi kuwa wana uhusiano mzuri na Mungu au la.
   - Uliza kama wangependa kuwa na uhusiano mzuri (bora) na Mungu.
   - Omba ruhusa ya kumshirikisha HADITHI YAKO (ushuhuda wako). Ikiwa wanakubali:


2. Shirikisha **HADITHI YAKO** (ushuhuda wako) ya:
   - Maisha yako yalivyokuwa kabla ya kumwamini Yesu,
   - JINSI ulivyokuja kuweka imani katika Yesu kama Mwokozi wako,
   - Jinsi maisha yako yalivyo tofauti BAADA ya kumwamini Yesu kwa Wokovu.
   - **Uliza**: *"Je, ungependa kujua jinsi unavyoweza kuwa na uhakika kwamba una uzima wa milele pamoja na Mungu?"*

3. Tumia *Zana ya Mishale 3 za Tumaini & Maisha* ***kujadili*** **HADITHI YA MUNGU** na mtu huyo.
   - Onyesha mistari kutoka **Yohana 3:16-18** na Alama Nne.
   - **Sema**: *"Aya hizi ni baadhi ya zinazojulikana sana katika Biblia na zinatuambia jinsi tunavyoweza kuwa na uzima wa milele pamoja na Mungu. Je, ninaweza kuyajadili na wewe?"*


**Muulize mtu huyo kama angesoma Yohana 3:16-18 kwa sauti.**

- Kuwa mwangalifu ikiwa hawawezi kusoma. Ikiwa wanasema kitu kama, "Sina miwani yangu," basi usome mistari kwa sauti.

4. Onyesha ishara ya **MOYO** (MUNGU) na **useme**:
   - Ishara hii inawakilisha Mungu. **Uliza**:
     - *"Unajifunza nini kuhusu Mungu katika mistari hii?"*
   - Sisitiza kwamba Mungu anapenda kila mtu ulimwenguni. **Uliza**:
     - *"Je, unaamini kwamba Mungu anakupenda?"*
     - *"Mungu alionyeshaje kwamba anaupenda ulimwengu?"* (Alimtoa Mwanawe pekee kwa ajili yetu.)
     - *"Mungu anataka nini kwa kila mtu ulimwenguni?"* (Ili wasipotee bali wawe na uzima wa milele)
   - Ikibidi, rejea mistari inayounga mkono kuhusu upendo wa Mungu kutoka sehemu ya #1 ndani ya zana.



5. Onyesha alama ya **WATU** na **useme**:
   - Ishara hii inaonyesha kwamba watu wametengwa na Mungu na upendo wake. **Uliza**:
     - *"Unafikiri ni kwa nini watu wametenganishwa na Mungu na hawana uzima wa milele pamoja naye?"*
       - Eleza kwamba ni kwa sababu ya dhambi zetu na kutomwamini Yesu, Mwana wa Mungu.
     - *"Ni hatari gani kwetu ikiwa tutaendelea katika dhambi na kutokuamini kwetu?"*
       - Eleza kwamba tutahukumiwa kwa sababu ya dhambi na kutoamini kwetu na hatutakuwa na uzima wa milele.
   - Ikibidi, rejelea mistari inayounga mkono kuhusu dhambi ya watu kutoka kwa nukta #2 ndani ya zana.



**Uliza mtu huyo (au wewe) kusoma mistari mara ya pili.**

6. Onyesha alama ya **MSALABA** na **useme**:
   - Ishara hii inawakilisha Yesu, Mwana wa Mungu, na kile alichofanya kwa ajili yetu. **Uliza**:
     - *"Unafikiri ni kwa nini Mungu alimtuma Yesu ulimwenguni?"*
       - Eleza kwamba sababu ilikuwa ni kufa badala yetu kwa ajili ya dhambi zetu.
     - *"Je, tunapaswa kuamini nini kuhusu Yesu ili tupate uzima wa milele?"*
       - Eleza kwamba Yeye ndiye Mwana pekee wa Mungu ambaye hakutenda dhambi kamwe, kwamba alikufa kwa ajili ya dhambi zetu ili tuweze kusamehewa, kwamba alifufuka kutoka kwa wafu na ndiye njia pekee ya kupata uzima wa milele pamoja na Mungu.
   - Ikibidi, tumia mistari inayounga mkono kuhusu Yesu kutoka sehemu #3 ndani ya zana.


7. Onyesha **ALAMA YA SWALI** (UAMUZI WAKO) na **useme**:
   - Kila mtu ana uamuzi kuhusu Yesu na zawadi ya uzima wa milele ambayo Mungu hutoa. **Uliza**:
     - *"Kulingana na mistari hii unapaswa kufanya nini ili kuwa na uzima wa milele pamoja na Mungu?"*
       - Ni lazima tuamini (kuweka imani yetu) katika Yesu kama aliyekufa badala yetu ili kusamehe dhambi zetu na ndiye njia pekee ya kupata uzima wa milele.
     - *"Unafikiri inamaanisha nini kuamini (kuweka imani yako) katika Yesu?"*
       - Kubali kwamba hii ni kweli.
       - Amini kwamba Yesu ndiye njia pekee ya kupata uzima wa milele.
       - Binafsi mtegemee Yesu pekee ili kumjua Mungu na kupata uzima wa milele.
     - *"Uamuzi wako ni upi? Je, ungependa kuweka imani yako kwa Yesu kukusamehe dhambi yako na kukupa uzima wa milele?"*
       - Wakisema "Ndiyo," waongoze kupitia maombi ya imani nyuma ya *ZANA*.
       - Hakikisha unawapa uhakika wa uzima wa milele kwa kuomba na kusoma **1 Yohana 5:11-12**.
       - Wakisema "Hapana," waulize kwa nini hawataki kuweka imani yao kwa Yesu. Fafanua mkanganyiko wowote nao kulingana na jibu lao.
   - Ikibidi, tumia vifungu vinavyounga mkono kutoka kwa nukta #4 ndani ya zana.

8. Hongera mtu huyo kwa imani yake mpya katika Yesu. Waambie kwamba huu ni mwanzo wa maisha yao mapya na kwamba ungependa kukutana nao tena ili kuwasaidia kukua katika imani yao mpya katika Kristo.
   - Omba kukutana nao siku inayofuata au haraka iwezekanavyo.
   - Andika wakati na mahali kwenye *ZANA*.
   - Andika majina yao na wakati na mahali pa kukutana nao kwenye sehemu ya kubomoa. Hifadhi hii kwako mwenyewe.
   - Mpe mtu huyo *ZANA* na umwombe asome mambo ya ndani kabla hamjakutana tena.

*"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye. Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu."*

Yoahna 3:16-18

**Kutoka kwa mistari hii, unajifunza nini kuhusu...**




FUNGA

**Sala ya imani:** *"Bwana Yesu, nakuhitaji. / Ninakiri kwako kwamba nimetenda dhambi dhidi yako na ninastahili hukumu ya milele. / Asante kwamba ulikufa na kufufuka ili kusamehe dhambi zangu zote. / Ninakuomba unisamehe na unipe uzima wa milele. Amina."*

**Je, kwa dhati uliweka imani yako kwa Yesu kukusamehe dhambi zako na kukupa uzima wa milele? Una nini sasa? (1 Yohana 5:11-12)**

Huu ni mwanzo wa maisha yako mapya na uhusiano wako na Mungu. Tungependa kukutana nawe tena ili kuzungumzia kutoka katika Biblia jinsi unavyoweza kukua katika uhusiano wako na Mungu. **Je, tunaweza kukutana lini kesho?**

Wakati _______________ Mahali ____________________________

FUNGA

Wakati ________ Mahali ________________

Vidokezo

Jina ________________________ Simu __________________

Anwani ____________________________________________

**1. Mungu anakupenda na anataka uwe na uzima wa milele pamoja Naye.**

- **2 Petro 3:9** - *"Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba."*
- **Warumi 5:8** - *"Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi."*

**2. Watu wote wametengwa na Mungu kwa sababu ya dhambi zao.**

- **Warumi 3:23** - *"... kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu."*
- **Warumi 6:23** - *"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu."*
- **2 Wathesalonike 1:8-9** -*Yesu atarudi... "katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu; watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake;."*

**3. Mungu alimtoa Mwanawe pekee mkamilifu ili afe badala yako ili kulipia dhambi zako.**

- **2 Wakorintho 5:21** - *"Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye."*
- **Yohana 14:6** - *"Yesu akamwambia, 'Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi.'"*

**4. Ni lazima uamini (weka imani yako) kwa Yesu kama njia pekee ya kukusamehe dhambi zako na kupata uzima wa milele.**

- **Yohana 1:12** - *"Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake."*
- **Waefeso 2:8-9** - *"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu."*
- **Warumi 10:9-10** - *"Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu."*

**5. Ukimtumaini Yesu pekee kama mwokozi wako anakupa uzima wa milele.**

- **1 Yohana 5:11-12** - *"... Na huu ndio ushuhuda, ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu umo katika Mwanawe. Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima."*

STRATEGIC IMPACT INTERNATIONAL

www.StrategicImpactInternational.com


© Permission to copy with attribution

3 Arrows Hope & Life Tool v3.0

# NANI?

Nani umshuhudie Injili rahisi kwa uwazi?
**KILA MTU** — lakini anza na wale ambao unamuunganiko nao.

1. Tumia jedwali hilo hapo chini ili **kuorodhesha** watu ambao unamuunganiko nao katika maisha ya **kila siku**. Miunganiko hii inaweza ikawa ya marafiki wa karibu au watu ambao munaonana mara kwa mara sokoni au maeneo mbalimbali, lakini huwajui majina yao.
2. Kwa muda wa wiki zima, **omba kila siku** kwamba Mungu afungue mioyo yao waisikie Injili.
3. **Tenga muda wa kuwaendea** (inaweza ikawa kwenye ratiba zako za kawaida) **washirikishe** mambo amabayo Mungu ameyafanya kwako, na washirikishe ujumbe rahisi wa Injili kwa kutumia *Mishale 3 Zana ya Tumaini na Maisha ya SI*.




- Uwe makini na watu ambao Mungu anawaleta kwenye maisha yako **kila siku** ili uweze kuwashirikisha Injili.

- Omba na kupambanua **kundi** au **mahali** munapoweza kwenda kuhubiri Injili.

## KIPINDI 5: *KIONGOZI ANATAKIWA KUFANYA NINI?*

**MAELEZO KWA UFUPI:**

**Lengo**: Mnenaji ataweka wazi maelezo ya kiongozi anatakiwa kufanya nini ili kuwashawishiwengine kutimiza Agizo Kuu.

**Kujua**: Viongozi wataelewa mambo muhimu anayofanya kiongozi.

**Kujisikia**: Viongozi watajisikia kukua katika ujasiri wa kuongoza.

**Mambo ya Kufanya:** Viongozi watumie ushawishi wa uongozi wao kuwasha moto wa mtembeo wa upandaji makanisa.

**Utangulizi:**

- Hitaji kubwa katika kanisa la leo ni viongozi wa kiungu ambao watawasha moto ndani ya kanisa ili kutimiza Agizo Kuu. Mungu anataka kukutumia wewe kuwashawishi watu wake ili kutimiza makusudi yake.
- Kiongozi wa Kikristo anatakiwa **kufanya** nini ili kuwashawishi watu wa Mungu kutimiza Agizo Kuu?

**1. Wanapandikiza MAONO**

A. Maono ya Mungu ya Agizo Kuu ni lazima yapandikizwe kwa wengine.

1. Watu wengi hawaangali nyuma. *"Mahali pasipo na maono watu wanaacha kujizuia."* (Mithali 29:18).

2. Kwa hiyo wajibu wa KWANZA wa kiongozi ni "**kuchora picha**" (Kama msanii) na kuonyesha mustakabali unaosema, "Huku ndiko tunakoelekea. Hivi ndivyo Mungu anavyotuita kutimiza Agizo Kuu."

3. Shabaha siyo kuwa na MAONO mengi lakini ni MAONO **pasipo wingi.** Hii inalipa shirika/taasisi muono/mkazo na inasaidia kushika jambo lililo Kuu.

**Maswali ya hiyari kwa washiriki** (Tumia maswali mengi kadri unayopata muda. Wagawe viongozi kwenye makundi ya watu 3 – 5 kwa ajili ya majadiliano, kisha mwakilishi wa kila kundi atashirikisha kundi lote.)
Omba mtu mmoja asome Mathayo 28:18-20, kisha ULIZA:
- Kwa kuangalia Agizo Kuu katika Mathayo 28:18-20, unaweza ukasema maono ya Mungu ni nini?
- Ni wapi tunakotakiwa kuwafanya wanafunzi? — kwa mataifa yote (angalia Matendo 1:8)

**2. Palilia KUAMINIWA**

A. Kuaminiwa ni **MKONDO** wa kweli wa kiongozi unaotokana na **TABIA**.

B. **Ufafanuzi wa kuaminiwa** - Ni hali ya kujua kwamba kiongozi atafanya wakati wote kwa maslahi ya shirika/taasisi na wanachama wake.

C. Kuaminiwa si jambo ambalo unaweza kulidai … bali UNAJIPATIA kwa tabia **ENDELEVU** na **NIA/DHAMIRA** njema.

D. Kuendeleza tabia ni suala la **maisha**. Huwezi kuhitimu.

E. Tabia ndiyo inayoamua hatima! Hivyo **WEWE** ulivyo Ni matokeo ya MAMBO unayofanya katika maisha (Luka 6:43- 45)!

3. **Toa MAAMUZI SAHIHI**
   A. UFAFANUZI: Kwa busara pambanua namna ya kutenda baada ya kutafakari katika Nyanja zote na kisha kwa ujasiri tenda kwa faida ya muda mrefu ya shirika/ Taasisi.

   B. Sehemu kubwa ya kujua unachotakiwa kufanya ni pamoja na kujua USICHOTAKIWA kufanya!

   C. Watu wako wanakutegemea wewe KUFANYA MAAMUZI MAZURI.

   D. Maamuzi mazuri yanaweza kuendelezwa kwa:
      - Matumizi ya maarifa ya Biblia.
      - Kwa hekima iliyopatikana kutokana na uzoefu.
      - Kutoka vyanzo mbali mbali, kwa watu wazima wenye busara. *"Pasipo mashauri makusudi hubatilika, Bali kwa wingi wa washauri huthibitika"* (Mithali 15:22).

4. **Kutenda KIMKAKATI**
   A. ANDAA na TEKELEZA mchakato wa kutimiza maono "Hatua 1, Hatua 2, Hatua 3, n.k."

   B. Kiongozi lazima atengeneze **Ramani ya barabara** ya kututoa "hapa" (mahali ulipo sasa) kwenda "kule" (mahali unapotakiwa kwenda).

   C. **Uongozi ni kujua**:
      1. Unachotakiwa kufanya,
      2. Kwa nini ni muhimu, na
      3. Namna ya kutumia rasilimali ili kukamilisha kazi.

**Maswali ya hiyari kwa washiriki** (Tumia maswali mengi kadri unayopata muda. Wagawe viongozi kwenye makundi ya watu 3 – 5 kwa ajili ya majadiliano, kisha mwakilishi wa kila kundi atashirikisha kundi lote.) Omba mtu mmoja asome Mathayo 28:18-20, kisha ULIZA:
- Yesu alikuwa na mkakati wa namna gani kutimiza maono ya kufikia Ulimwengu? —> "kuwafanya wanafunzi"
- Ni mikakati gani 3 ambayo Yesu anatupa ya kuwafanya mataifa kuwa wanafunzi? —> "nenda"; "batiza"; "wafundishe kutii"
  - Nini maana ya "nendeni"?
  - Nini maana ya "kubatiza"?
  - Nini maana ya "kuwafundisha kutii"?

5. **KUWAWEZESHA WENGINE kutimiza Maono!**
   A. Kipimo cha kiongozi wa kweli siyo kwa Yale anayoyafanya, bali kwa yale ambayo **wengine** wanayakamirisha kutokanana alichokifanya kwao!

   B. Kiongozi wa kweli anawaendeleza wengine na kisha kuwaachilia kutimiza Maono ya Mungu.

**MAMBO YA KUFANYA*:***
1. Kutokana na orodha hiyo hapo juu, chagua sifa mbili za uongozi unazotaka kuendeleza ndani yako mwenyewe kwa miezi sita ijayo ili kuhakikisha kwamba unawashawishi wengine kutimiza Agizo Kuu.

2. Ni kwa jinsi gani mahususi utaweza kuendeleza hazina hizi muhimu?

## KIPINDI 6: *TABIA: JIWE KUU LA PEMBENI LA KIONGOZI WA KIKRISTO*

**MAELEZO KWA UFUPI:**

**Lengo**: Mnenaji ataonyesha kwamba tabia/uadilifu ni msingi muhimu wa kiongozi wa Kikristo.
**Kujua**: Viongozi waelewe kwamba tabia ya kiungu ni sifa yenye kipaumbele kwaviongozi wa Kikristo.
**Kujisikia**: Viongozi washawishike kushughurikia dhambi za siri kwenye maisha yao.
**Mambo ya Kufanya:** Viongozi watubu na kuacha dhambi za siri na wawajibike kwa Wakristo wenzao.

**Utangulizi:**

**Mapendekezo ya kielelezo cha mfano wakati wa ufunguzi mbele ya wanakongamano**

- Wangapi wenu mnapenda ndizi (au chagua tunda ambalo ni maarufu kwenye hilo eneo)?
- Wacha tuseme umechagua ndizi nzuri, yenye rangi ya manjano bila madoa kwa nje, menya hiyo ndizi, kisha ing'ate hiyo ndizi halafu angalia katikati ya hiyo ndizi halafu unaona jamii ya mdudu (kama kunguni) akitambaa.
- Je utaendelea kula hiyo ndizi? Kwa nini?
- Viongozi wengi ni kama ile ndizi nzuri ya manjano kwa mwonekano wote wa nje wana vyeo vikubwa, elimu, maarifa, uzoefu na ujuzi – lakini wanakosa sifa za ndani za kiongozi yaani tabia.
- Kwa nje wanaonekana vizuri. Lakini kwa ndani kuna kitu kimeoza.

◉ Kuna viongozi wengi wakubwa katika ulimwengu huu wenye karama, maono, ushawishi na ujuzi (ustadi). Lakini kama unazo sifa hizi halafu umepungukiwa — tabia ya kiungu — huwezi kuwa kiongozi wa Kikristo kwenye kanisa.

◉ Unaweza ukawa na msukumo wa maono ya Agizo Kuu na kuwashawishi wengine lakini …

**1. Huwezi kuwa kiongozi wa Kikristo bila kuwa na TABIA ya kiungu.**

A. Mungu anapotafuta viongozi Anaangalia **tabia** kama sifa ya kwanza.
(1 Timotheo 3:1-7; Tito 1:5-9; 1 Samweli 16:7)

1. Sifa ZOTE za kuwa mwangalizi katika kanisa la Kristo zinaongelea tabia — kasoro mbili tu — zinaongelea wewe ulivyo ndani ya Kristo.

2. Ujuzi PEKEE uliongelewa kwenye orodha hii ni "Uwezo wa kufundisha" na "kuisimamia nyumba yako vizuri."

B. Tabia ni "**kudhihirisha** maisha ya Kristo" na ni **muhimu** ili utimize misheni yetu ya kuwafanya wanafunzi wanaojizidisha.
(Wafilipi 3:17; 1 Wathesalonike 1:6-9; 1 Wakorintho 4:1-2, 11:1; 2 Timotheo 2:2)

1. Tabia ya kiungu ni matokeo ya maisha ya **Yesu yanayozaliwa ndani yetu**.
   a) Tabia inazaliwa ndani yetu na Roho Mtakatifu anapotubadilisha ili kufanana na Yesu na tunapofuata maelekezo yake (2 Wakorintho 3:18; Wagalatia 5:16-18).
   b) Tabia inadhihirishwa kwa tunda la Roho Mtakatifu ndani yetu (Wagalatia 5:22-26).
   c) Tunakuwa katika tabia ya Kristo tunapokaa ndani ya Kristo (Yohana 15:1-8).
   d) Tabia siyo matokeo ya kujibadirisha wenyewe bali badiliko tunalopata kwa msaada wa Roho Mtakatifu (Warumi 12:1-2).
   e) Njia bora ya kukua katika tabia ya Kiungu ni kuendelea kujazwa na kutembea na nguvu za Roho Mtakatifu.

2. **Asili** ya huduma yetu ni kutengeneza maisha ya Kristo kwa wengine ambao nao watafanya hivyo hivyo kwa wengine, na kadharika.

3. Kama maisha ya Kristo hayatakuwa ya mfano, kwa sisi **kuyasababisha** yatokee kwa wanafunzi tunaowaandaa, basi mchakato wa kujizidisha utabomoka. **Uhalali wa ukristo wetu hautaweza kutamanisha wengine** (1 Wakorintho 11:1).

4. Watu wa Mungu hawawezi kumfuata kiongozi kama hawawezi **kumwamini**.

Ndiyo maana *Maswali ya ya Kukua Kiroho* (1-3) ni muhimukwenye *Timu Yasafari*. Yanalenga tabia na kutuonyesha maeneo ambayo tunahitaji kumruhusu Roho Mtakatifu atubadilishe katika maisha yetu!

**2. Tabia ni MWENDELEZO — wa kuwa mwanaume/mwanamke wa kimungu kila mahali na unapokuwa na mtu yeyote.**

A. UFAFANUZI: **Tabia** — "Kuaminiwa kunakotokana na kudhihirisha **uadilifu**."

1. Tabia ya kiungu ya Kikristo inatokea pale ambapo **ujumbe** wako unapoendana na **tabia**, wewe unakuwa vile unavyokiri kuwa (Zaburi 15).

2. Tabia ya kiungu ya Kikristo inatokea wakati **moyo** wako unapoendana na **maneno** yako (Zaburi 17:1-3).

3. Tabia ya kiungu ya Kikristo ni kinyume cha **unafiki** — kujifanya uko hivi wakati kumbe wewe ni kitu kingine kabisa (Luka 11:37-12:2).

4. Tabia ya kiungu ya Kikristo haina mambo ya **siri**.

5. Tabia ya kiungu ya Kikristo haimaanishi **ukamilifu**, bali inamaanisha **maendeleo** (1 Timotheo 4:15-16).

**3. Kuna maeneo nyeti manne ambayo viongozi wa kikristo wanatakiwa kukuwa katika tabia ya kiungu:**

A. **Ulimi** wako: **Fanya** ulichosema utafanya (Zaburi 15:2-4; Yakobo 3:1-2).
B. **Fedha**: "Jiepushe na roho ya **kupenda** fedha" (Zaburi 15:5; 1 Timotheo 6:6-11).
C. **Ngono**: "**Ikimbie** zinaa" (1 Wakorintho 6:18-20).
D. **Madaraka/Nguvu**: "Tafuta **kutumika** na siyo kutumikiwa" (Marko 10:42-45).

**Huwezi Ukawa Kiongozi Wa Kikristo Aliyefanikiwa Bila Kuwa Na Tabia Ya Kiungu.**

**MAMBO YA KUFANYA:**

1. Je kuna dhambi yoyote ya siri kwenye maisha yako? Mungu anakuita kutubu na kuiacha leo. Unapotafakari tabia ya Yesu, ni msimamo gani wa kiimani, maadili, mitazamo, na matendo ambayo Roho Mtakatifu anakuongoza kubadilika ili kufanana na yeye? **Sasa ni wakati wa kutubu.**

2. Muombe Roho Mtakatifu aanze kuibadilisha tabia yako katika maeneo mbali mbali ili ufanane na Kristo. Shikamana na Roho Mtakatifu ili ukue katika tabia ya kiungu kama anavyotaka uwe (Wagalatia 5:16-22).

3. Tabia ya kiungu inatengenezeka na kubadilika tunapowakaribisha waumini wachache tunaowaamini ili tuwajibike kwao. Utaanza lini kukutana nao kwenye timu ya *Maswali ya ya Kukua Kiroho* ili muulizane maswali ya kubadilisha maisha (Waebrania 10:24-25).

## KIPINDI 7: *MZIGO NA UPENDO KWA AJILI YA KRISTO NA WALIOPOTEA*

**MAELEZO KWA UFUPI:**

**Lengo**: Mnenaji atawasaidia viongozi ili **kukutana** na ile shauku na upendo wa Mungu kwa ajili yao.

**Kujua**: Viongozi **wataelewa** upendo wa Mungu kwa ajili yao na kuitikia kumpenda Mungu na watu waliopotea katika dhambi.

**Kujisikia**: Viongozi **wataitikia** kwa kurudisha upendo kwa Mungu.

**Mambo ya Kufanya**: Viongozi watajitoa **kupeleka** upendo wa Mungu wenye mzigo kwa wale wasiomjua Kristo.

**Utangulizi:**

◉ Kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya:
- Upendo wetu **kwa Kristo** na
- Mzigo/Upendo tulionao kuufikia **ulimwengu uliopotea**.

◉ Mzigo wako wa kufanya uinjilisti kwa kizazi chetu UNA UWIANO WA MOJA KWA MOJAna upendo wetu kwa Kristo.
- Mungu anataka viongozi wa kikristo kumtii, lakini utii pekee hauwezi kutupa hamasa ya kuwafanya wanafunzi wanaojizidisha ili kutimiza Agizo Kuu.
- Hamasa pekee itakayotusaidiwa kuvumilia ni pendo letu kwa Kristo linalobubujika kuwafikia watu waliopotea.
- Kadri tunavyompenda Yesu, ndivyo tunavyozidi kuwa na shauku yakutaka waliopotea wamwamini yeye kwa ajili ya wokovu.

**Maswali ya hiyari kwa washiriki** (Tumia maswali mengi kadri unavyopata muda — fanya hivyo)
- Mtu mwenye kiu, nikimpa bilauli (glasi) tupu, je, hii itakidhi au kuondoa kiu yake?
- Ni pale tu nitakapojaza maji kwenye Bilauli na kumpa mtu ndipo anapoweza kumaliza kiu yake.
- Kama sijajazwa na upendo wa Mungu, Sina kitu cha kumpa mtu mwingine hivyo utakuwa ni utii mtupu, usio na kitu.
- Nikijazwa upendo wa Mungu, upendo wa Mungu ndio unaotiririka kupitia mimi kwenda kwa wengine.

◉ SWALI: Ni jinsi gani tunakuwa katika pendo letu kwa Kristo na mzigo kwa waliopotea?

◉ Kuna hatua 3 ili kupata mzigo wa kutimiza Agizo Kuu:

**1. POKEA upendo wa shauku wa Mungu kwako:**

A. ASILI ya Mungu ni UPENDO — Huu ndio UNDANI wa jinsi alivyo.

B. Mungu ni Baba mwenye upendo anayetaka “kuumimina” upendo wake kwako:

1. *“Kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwakatika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi.”* (Warumi 5:5b)

**Maswali ya hiyari kwa washiriki** (Tumia maswali mengi kadri unavyopata muda. Wagawanye viongozi kwenye makundi ya watu 3- 5 kwa ajili ya majadiliano, kisha mwakilishi wa kila kundi ashirikishe kundi lote.) ULIZA:

- Mungu amemimina nini ndani ya moyo wa kila mtu anayemwamini Yesu?
- Nini matokeo ya kuwa na upendo wa Mungu ndani yetu?
- Ni jinsi gani Mungu anamimina upendo wake ndani ya mioyo yetu?
- Ni kitu gani kinachomuhamasisha Mungu kufanya hivyo?

2. Mungu anakupenda sana kiasi kwamba hakuna kitu kinachoweza kukutenga na upendo wake mkamilifu:
    a) *"Ni nani atakaye tutenga na upendo wa Kristo? Je ni dhiki, au shida, au adha, au nja au uchi, au hatari, au upanga?"* (Warumi 8:35)

3. Watu wa Mungu ni ***"mboni ya jicho la Mungu."*** (Zaburi 17:8)

**Maswali ya hiyari kwa washiriki** (Tumia maswali mengi kadri unavyopata muda. Wagawanye viongozi kwenye makundi ya watu 3- 5 kwa ajili ya majadiliano, kisha mwakilishi wa kila kundi ashirikishe kundi lote.) ULIZA:

- Mtunga Zaburi anamuomba Mungu amfanyie nini?
- Maana yake nini kuwa "mboni ya jicho la Mungu" (Usemi wa mboni ya jicho – ni mkazo ambao Mungu anakuwa nao juu ya mtu).?

4. Wewe ***"unaheshimika na ni wathamani machoni pake."*** (Isaya 43:4)

**Maswali ya hiyari kwa washiriki** (Tumia maswali mengi kadri unavyopata muda. Wagawanye viongozi kwenye makundi ya watu 3- 5 kwa ajili ya majadiliano, kisha mwakilishi wa kila kundi ashirikishe kundi lote.) ULIZA:

- Ni jinsi gani Mungu anaeleza upendo wake kwa watu wake?
- Maana yake nini kuwa wa "thamani"? na "kuheshimiwa"?
- Kama matokeo ya upendo wake kwetu Mungu anataka kufanya nini?

5. Kama Mungu angesema kwa sauti ya wazi kwako leo moja ya vitu ambavyo angesema ni hili:
    "Wewe ni **FURAHA** ya moyo wangu."

Swali la Utendaji: Je unaweza **kuufungua moyo wako** kwa Baba leo,
na **KUPOKEA** upendo wa Mungu kwa ajili yako?

[Wape nafasi viongozi wakae kimya katika hali ya kuomba mbele za Bwana.]

Hatua ya KWANZA ni kupokea upendo wa Mungu kwa ajili yako, hatua ya PILI ni…

**2. ITIKIA kwa kumrudishia Mungu upendo:**

A. Moja ya vitu vya asili katika ulimwengu ni **kuitikia** upendo kwa **kutoa** upendo.

1. Biblia inasema: *"Sisi twapenda **kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza.**"* (1 Yohana 4:19)
2. Sababu pekee inayotupa uwezo wa kumpenda Munguni **MWITIKIO** wa **upendoaliouanzishakwanza**.

B. Mfano: AMRI KUU
   1. Je unakumbuka Yule mwanasheria alivyomuuliza Yesu:
      *"Mwalimu, ni amri ipi iliyo kuu?"* (Mathayo 22:36)

      Yesu alifafanua kwamba:
      *"Mpende bwana mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako na kwa akili zako zote na ya pili yafanana nayo nayo ni hii "mpende jirani yako kama nafsi yako."* (Mathayo 22:37-39)

C. Mambo ya kufanya: **Matumizi mazuri ya maisha ni UPENDO**.
   1. **Maisha yana nini?** Ukifikiri juu ya maisha unaweza kusema kwa ufupi kuhusu maisha kama:
      a) KUPOKEA upendo wa Mungu,
      b) KURUDISHA upendo kwa Mungu:
      c) KUWAPA wengine upendo wa Mungu.

**3. PELEKA/AMBUKIZA upendo wa Mungu kwa watu wasiomjua:**

A. Tunapopokea upendo wa Baba kwa ajili yetu na **kuitikia** kwa kumrudishia Mungu upendo. **Hii itapelekea/ambukizo la kuwapenda** watu waliopotea (jirani zako).

B. Mtume Paulo alisema: *"Maana upendo wa Kristo* ***watubidisha****."* (2 Wakorintho 5:14)
   Tafsiri nyingine inasema: *"Upendo wa Kristo* ***umetushika****."*

C. Tunapompenda Yesu kweli pendo lake linatupeleka na kutusukuma kwa waliopotea. *"Kwa kuwa mwana wa Adam amekuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea."* (Luka 19:10)

D. Ni pendo la Kristo kwa roho zilizopotea ndilo linalotusukuma**kumueleza** kila mtu mwenye utayari wa kusikiliza injili. **Upendo kwa Kristo** unatupeleka kuwa na **mzigo wa roho zilizopotea**.

E. **UPENDO** wetu kwa **Kristo** utapelekea **kuwapenda waliopotea.**

   1. Mwombe Mungu akupe mzigo wa roho zilizopotea.

   2. Mungu anakualika uishi maisha yenye Pendo la moto kwa ajili ya Kristo — na kutokana na huo moto kwa kumpenda Kristo uwe na shauku na upendo kwa waliopotea!

**HITIMISHO:**
- Nataka "KULEWA" upendo wa Bwana Yesu — Nataka "NIFURAHISHWE" na uzuri wake!

- Na kutokana na "Kulewa" upendo wa Bwana Yesu nataka kuyatoa maisha yangu yote kuwafikia waliopotea kwa upendo wa Kristo.

**MAMBO YA KUFANYA:**
Kaeni kwenye makundi ya watu 2 au 3 na kisha ombeni mambo haya:

3. "Bwana nijaze kwa upya upendo wako."
4. "Bwana narudisha upendo kwako katika hali ya kukuabudu."
5. "Sasa Bwana nauachilia upendo kwa watu walionizunguka."

***Strategic Impact - Uzinduzi wa Kiongozi***
**Mkakati wa Kuufikia Ulimwengu Wako Ulipoptea**
***Hatua 7*: Wafundishe Wanafunzi Wapya Walioamini**

**MAELEZO KWA UFUPI:**

**Lengo**: Mnenaji atapitia *Hatua 10 za Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea* na kuelezea vizuri *Hatua 7*.

**Kujua**: Viongozi wataelewa kabisa umuhimu wa ufuatiliaji na mafunzo ya waamini wapya.

**Kujisikia**: Viongozi watajisikia umuhimu wa kuhusika katika kuwafanya wengine kuwa wanafunzi.

**Mambo ya Kufanya**: Viongozi watajitoa kuwalea/ kuwafundisha wale waliowaongoza kumpokea Kristo. Kwa wakati huu viongozi waonyeshe alama 7 za mikono katika zile *Hatua 10* na kuweza kuzisema kwa mtu yeyote wakati wowote.

## Hatua 7: Wafundishe Wanafunzi Wapya Walioamini

Wafundishe waamini wapya mahali au katika eneo lao ulilowakuta. (Matendo 14:22; 20:20)

A. Pitia *Hatua* 7 za Mwanzo na alama za mikono kwa kila.

B. Baada ya kumuongoza mtu katika imani ya Yesu, ni muhimu kumfundisha mwamini mpya.

C. Kwenye kipindi cha 6 tutajadili kuhusu asili ya mafunzo ya uanafunzi na kukukabidhi zana ya kuzaa wengine ili ikusaidie wewe na Timu yako kuwafundisha waamini wapya.

## KIPINDI 8: *ASILI YA UANAFUNZI: WAFUNDISHE WANAFUNZI*

**MAELEZO KWA UFUPI:**

**Lengo**: Mnenaji atatambulisha dhana ya uanafunzi kwa waamini wapya na kufundisha jinsi yakutumia maswali 6 ya ufuatiliaji yaliyo nyuma ya *ZANA YA UKUAJI NA KUZIDISHA YA SI*na 5 hatua za mchakato wa uanafunzi kutoka kwenye *ZANA YA UKUAJI NA KUZIDISHA YA STRATEGIC IMPACT*.

**Kujua**: Viongozi wataelewa kwamba kuwaandaa wanafunzi ni mchakato wa maisha wa kudhihirisha na kusaidia wengine ili wakue na kuzidisha wanafunzi.

**Kujisikia**: Viongozi wataelezwa juu ya umuhimu wa kuwafundisha waamini wapyammoja mmoja au kupitia vikundi vya watu 2-5.

**Mambo ya Kufanya:** Viongozi watajitoa binafsi kuwafuatilia wale waliowaongoza katika imani kumpokea Kristo.

**Utangulizi:**

**Mapendekezo ya kielelezo cha mfano wakati wa ufunguzi mbele ya wanakongamano**

- Mtoto mchanga anapokaribia kuja, kunakuwa na furaha kadri siku zinavyosogea, kisha kuna furaha siku mtoto akizaliwa na wakati wa kumbeba mikononi.
- Baada ya hapo unafanya nini? Je utamwacha mtoto hospitali au utamtelekeza baada ya kuzaliwa?
- Je utajadiliana na mwenzi wako juu ya furaha ya kupata mtoto halafu mnamwacha mtoto hospital au mnamtelekeza?
- Ni ujinga kwetu ikiwa tutafanya uinjilisti kwa mtindo huu – yaani unawaongoza watu kufanya maamuzi ya kumpokea Yesu halafu unawatelekeza hivyo hivyo.

◉ Ukiwashishirikisha watu wengine injili kwa uaminifu, kutakuweko na wale ambao wataitikia na kumwamini Kristo kama mwokozi wao.

◉ Ni jambo muhimu kuwajenga hawa waamini wapya katika imani yao ndani ya Kristo, kisha wasaidie kukua na kuzidisha wanafunzi. Hii ni tofauti na kuwahubiria au kuwaweka tu kanisani. Huu ndio wakati wa kujenga mahusiano ya kuwafundisha waumini wapya ili waweze kuimarishwa katika mafundisho ya msingi ya Imani.

**UMUHIMU WA KUWAFUNDISHA WAAMINI WAPYA**

1. **Lazima TUWATEMELEE waamini wapya na kuwafundisha huko huko wanakoishi, wanakofanya kazi, kwenye shughuri zao za kila siku.**

   Tunatakiwa **tuwafuate** na tusitegemee wao watufuate. Wafundishe waamini wapya mmoja mmoja au kwenye vikundi vidogo vya watu 2 mpaka 5.

**NYENZO YA UANAFUNZI YENYE KULETA MATOKEO**

2. **Anza kwa kutumia mwongozo na topiki 4 "Msingi" za kuwatembelea mara 4 kutoka kwenye *ZANA YA UKUAJI NA KUZIDISHA YA SI*(Angalia kipindi saba 7B — "Jinsi ya kutumia kipeperushi au *ZANA YA UKUAJI NA KUZIDISHA YA SI*").**

   A. **Ikiwezekana**, watembelee waamini wapya ndani ya masaa 48 baada ya mtu kuokoka.

   B. **Ikiwezekana**, wape Injili ya Mtakatifu Yohana ili waanze kuisoma.

3. **Baada ya kuwatembelea mara 4 wanafunzi waaminifu waendelee kukutana na wewe kwa mafundisho zaidi ya kukua kiroho na uanafunzi.**

   A. Ikiwezekana, wapatie Biblia Agano Jipya kama zawadi siku ya kuhitimu mafundisho ya vipindi 4 ulivyowatembeleakatika awamu ya kwanza.

   B. Waombe waendelee kukutana na wewe ili waendelee kukua katika imani kwa kuwafundisha kutoka kwenye *Zana ya Ukuaji na Kuzidisha ya SI*.

**HITIMISHO:**

- Haitoshi tu kufanya uinjilisti na kuwasaidia watu kumkiri Kristo kwa Imani. Yesu hakutuamuru kwenda kujaza fomu za watu walioamua kuokoka bali alitutuma "kuwafanya mataifa kuwa wanafunzi."

- Haitoshi tu kuwaarika waamini wapya kanisani kwako; lazima uwasaidie kukua katika imani yao ndani ya Kristo. Ni lazima tutoe uangalizi kwa waamini wapya ili kuwasaidia kukua na kuzidisha wanafunzi

- Je wewe na timu yako mtakuwa tayari kujitoa kuwafanya wengine kuwa wanafunzi na kuwaongoza katika imani?

***Strategic Impact - Uzinduzi wa Kiongozi***
**Zana: *Jinsi Ya Kutumia Zana ya Ukuaji na Kuzidisha ya SI***

## Fuata Hatua 5 Za Maendeleo Ya Msingi Munapokutana Pamoja

1. **MAHUSIANO**: Waulize wanaendeleaje na tafuta yaliyojiri katika maisha yao tangu mlipoachana kwenye mkutano wenu wa mwisho.

2. **KUTIA MOYO**: Anza kipindi kwa kujibu ***Maswali ya Kukua Kiroho*** (yanayotokana na Wagalatia 5:22-23): **Wiki hii…**
   a. Je umejikabidhi kwa Roho Mtakatifu na kutunza upendo wenye shauku kwa ajili ya Yesu?
   b. Je umetembea katika upendo, amani, wema na msamaha katika mahusiano na familia, marafiki, waamini wenzio, majirani na maadui zako?
   c. Je umekuwa katika upendo na ibada kwa ajili ya Kristo Wiki hii? Kwa namna gani?
   d. Je umekuwa na kiasi na kumheshimu Kristo kwenye michakato yako ya kifedha?
   e. Je umejizuia dhidi ya mawazo ya ngono na matendo yake au je umezoelea tabia yoyote ambayo inaleta vifungo?
   f. Je umekuwa mwaminifu kuwashuhudia waliopotea na kuwafundisha wengine? Nani hao?
   g. Je umekuwa mwaminifu kusoma Biblia na kutimiza mambo **mliyokubaliana kufanya** wiki hii?

3. **KUJADILIANA**: Someni na mjadiliane vifungu vya Biblia vilivyoainishwa katika kila safari kwa kutumia **Maswali 6** (kama ilivyoelekezwa kwenye *Zana ya Kipeperushi Cha Uanafunzi ya SI*)
   a. Hakikisha kila mtu anajisikia vizuri kujadiliana maswali kwa kufuata Biblia. [**ZINGATIA**: Hapa **sio** mahali pakutoa ujumbe. unawasaidia waamini wapya namna wanavyoweza kujifunza Biblia kwenye maisha **yao**.]

## MASWALI 6

Mmoja na asome kifungu husika kwa sauti wakati wengine wanasikiliza au wanasoma wakifuatilia tokea kwenye Biblia.

Uliza maswali mawili ya awali na waruhusu waendelee kujadiliana na kupeana mawazo:

1. *Umepanda nini kutoka kwenye kifungu hiki?*
2. *Kitu gani hujapenda, au umeona kina changanya, kuhusiana na habari au kifungu hiki?*

Kusoma kifungu tena. Kujadili ijayo maswali mawili:

3. *Je, wewe kujifunza kuhusu watu kutoka katika kifungu hiki?*
4. *Je, wewe kujifunza kuhusu Mungu kutoka katika kifungu hiki?*

Baada ya muda wa majadiliano, mmoja asome kifungu kile kwa mara ya tatu kwa sauti na kisha jadilianeni maswali ya mwisho:

5. *Kulingana na kifungu hiki maisha yako yanawezaje kubadilika wiki hii? Uwe dhahili tambua. (Andika majibu ya watu na kisha mtakapokutana tena waulize maendeleo yao kulingana na majibu yao haya.)*
6. *Unamfahamu na mwingine anayehita kujua hadithi au kifungu hiki? (Taja jina, na sema kwa nini na lini utakapo mshirikisha au kumwambia.)*

   b. Pitia **somo** la **Safari 1**: “Yesu ni nani?” na maandiko yake Yohana 14:1-18.

   c. Ukimaliza somo la kwanza somo la kutembelea safari 1, wewe na waamini wapya mutakuwa muyasoma mafungu ya maandiko hayo ya Biblia **mara 3**.

   d. Ninyi nyote mtakuwa mmejibu maswali yote ya kwanza 4 ambayo yatakuwa yamewasaidia.

   e. Ninyi nyote mutakuwa mumejitoa kutii kutenda makubaliano kutokana namlivyojifunza kuwashirikisha wengine habari za Yesu.

   f. f) Katika safari inayofuatamuwe na uhakika wa kufuatilia kila mmoja kulingana na namna mlivyotii na kutimizamakubaliano mliyoyafanya kwenye swali la 5 na lile la 6 la kujitoa kufanya uinjilisti.

## ZIARA ZA MSINGI

**1:** Yesu ni nani?
*Yohana 14:1-11*

**2:** Maisha Mapya na Upendo wa Mungu.
*Yohana 3:1-18*

**3:** Uwe na uhakika wa wokovu wako.
*Yohana 10:27-30*

**4:** Kukaa ndani ya Yesu.
*Yohana 15:1-11*

g. Kuna topiki zingine tatu na maandiko yaliyotolewa kama **Safari ya Msingi** kwa wanafunzi wa baadae. Ni muhimu kukumbuka kwamba lengo ni kuwasaidia waamini wapya kuweza kusoma, kuelewa na kuitii Biblia wakiwa wenyewe wanapoendelea kukua katika uhusiano wao na Yesu na waamini wengine.

h. Baada ya **Safari nne za Msingi**, ni wakati mzuri kutulia na kufanya tathimini ya maendeleo ya waamini wapya na kufanya maamuzi ya kuendelea na **Safari za Kuwasaidia Kukua** kiroho au la. Kama wamekuwa waaminifu kuendelea kukutana, na wamekuwa katika uaminifu wa kutunza kwa uaminifu kutekeleza makubaliano ya kila wiki, na kama wamemshirikisha mtu mwingine habari za Yesu, hapo unaweza kuendela kuwafundisha masomo ya kukua kiroho na kisha uwalete kanisani

4. **MPANGO**: Kubalianeni maandiko ya kwenye Biblia ambayo kila mtuatasoma wiki hii. (tunashauri Sura 3 kwa siku).
   a. Uwe makini kwa wale wasiojua kusoma.
   b. Wapatie Biblia ya sauti kama ipo.
   c. Hakikisha unaandika kwenye karatasi majibu kutokana na Swali la 5 na 6 ili kufuatilia kwenye safari ya kutembelea inayofuata.
   d. Panga safari inayofuata ya kuwatembelea wanafunzi.
   e. Angalia wale waliotayari kushiriki na waliojitoa kusoma nyumbani na kujifunza zaidi kuhusu Kristo na kuwashuhudia wengine habari za Yesu. Hawa ndo watu unaotakiwa kuendelea nao kuwafundisha na kuhusiana nao hata baada ya kuwatembea Safari 4.

5. **OMBA**: Malizia muda wa kukutana nao kwa maombi ya pamoja mkiombeana kila mtu na mwenzie na kuombea mipango mliofikia kutokana na Maswali ya 5 na 6.

**SI**

**ZANA YA UKUAJI NA KUZIDISHA**

V3.0

STRATEGIC IMPACT INTERNATIONAL

S.L.P. 78640 · Dar es Salaam, Tanzania
www.StrategicImpactInternational.com
© Jisikie huru kunakili na SI inayohusishwa

## HATUA 5

1. **HUSIKA**: Waulize wanaendeleaje na tafuta yaliyojiri katika maisha yao tangu mlipo achana kwenye mkutano wenu wa mwisho.
2. **TIA MOYO**: Anza muda wako kujibu maswali ya Ukuaji wa Kiroho (kulingana na Wagalatia 5: 22-23). **Wiki hii…**
   A. *Je! Umejitiisha kwa Roho Mtakatifu na kudumisha upendo wa shauku kwa Yesu?*
   B. *Je! Umetembea kwa upendo, amani, uvumilivu, fadhili, na msamaha katika uhusiano wako na familia, marafiki, waamini wenzako, majirani, na maadui?*
   C. *Je! Umekua katika upendo wako na kujitolea kwa Kristo wiki hii? Vipi?*
   D. *Je! Ulijidhibiti na kumheshimu Kristo katika shughuli zako za kifedha?*
   E. *Je! Ulijidhibiti mwenyewe juu ya mawazo na matendo ya ngono, na tabia yoyote ya uraibu?*
   F. *Je! Ulikuwa mwaminifu kuwashuhudia waliopotea na kuwafuata wengine? WHO?*
   G. *Je! Ulikuwa mwaminifu kukamilisha usomaji wako wa Biblia na ahadi za "NITATAKA" wiki hii?*
3. **JADILI**: Soma na jadili kifungu cha Biblia mlichokuwa mmepeana mlipokutana kwa kufuata mfumo wa maswali 6 yafuatayo.
4. **MPANGO**: Pataneni kipengele cha maandiko matakatifu mtakayosoma wiki ijalo. (imependekezwa sura 3 kwa siku).
5. **OMBA**: Malizia muda wenu wa kukutana kwa maombi ya pamoja mkiombeana kila mtu na mwenzie na kuomba mipango mlioifikia kutokana na mswali va 5 na 6.

### *Strategic Impact - Uzinduzi wa Kiongozi*
### *Mkakati wa Kuufikia Ulimwengu Wako Ulipoptea*
### *Hatua 8*: Wakusanye Waamini Wapya

**MAELEZO KWA UFUPI:**

**Lengo**: Mnenaji atapitia *Hatua 10 za Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea*.
**Kujua**: Viongozi wataelewa *Step 8* kati ya *Hatua 10 za Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea*.
**Kujisikia**: Viongozi watajisikia hamasa ya kukusanya waamini wapya kwenye kanisa jipya lililopandwa.
**Mambo ya Kufanya**: Viongozi watajifunza alama za mikono za *Hatua 10 za Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea* na kuweza kusema kwa kila mtu wakati wowote.

**Utangulizi:**

- Pitia *Hatua* 7: waambie viongozi wasome hizo *Hatua* baada yako kwa kuonyesha alama za mikono katika kila *Hatua*.

- Wakati wewe na timu yako munapofanya uinjilist (*Hatua 6*) na kuwafundisha waamini wapya (*Hatua 7*) mahali walipo katika maeneo yao mulipochagua kupanda kanisa, *Hatua* inayofuata…

## Hatua 8: Wakusanye Waamini Wapya

*Kukusanya waumini wapya pamoja kwa vipaumbele vinne vya huduma ya kanisa:*

A. Kuabudu (Matendo 2:42-43; 1 Corinthians 14:26-35; 16:1-2; Wakolosai 3:16),
B. Ukuaji (Matendo 2:42; Wakolosai 4:16; 2 Timotheo 4:2),
C. Ushirika (Matendo 2:44-46; 8:35-38; Waefeso 4:11-16),
D. Unjilisti (Matendo 2:47; 5:42; 8:4; 19:10; Wafilipi 2:15-16).

A. Wakusanye waamini wapya ili kuanza kanisa.

B. Kanisa ni nini? Kanisa siyo jengo. Kwa maneno rahisi, **kanisa ni kusanyiko la wafuasi wa Kristo wanaoongozwa na kiongozi wa kiroho mwenye sifa, chini ya mamlaka ya Biblia. Watu hawa hukusanyika mara kwa mara ili kumuabudu Mungu, kukua kiroho, kupendana na kutumikiana, na kuwafanya wanafunzi wanaojizidisha katika ulimwengu uliopotea.**

C. Lengo lenu siyo kupanda kanisa jipya bali kupanda makanisa yanayojizidisha.

D. Shabaha yenu iwe ni kuwafanya wanafunzi wanaojizidisha ambao watapanda makanisa yanayojizidisha na kwenda kuwafanya waaminio kuwa wanafunzi hadi kila mtu asikie habari za tumaini pekee La uzima wamilele ndani ya Yesu!

**MAELEZO KWA UFUPI:**

**Lengo**: Mnenaji atapitia *HATUA 10 ZA KUFIKIA ULIMWENGU WAKO ULIOPOTEA*.

**Kujua**: Viongozi wataelewa *HATUA YA 9* ya *HATUA 10 ZA KUFIKIA ULIMWENGU WAKO ULIOPOTEA*.

**Kujisikia**: Viongozi watapata changamoto ya kuguswa kuwafundisha viongozi wanaojizidisha watakao panda makanisa mapya yanayojizidisha.

**Mambo ya Kufanya**: Viongozi watajifunza alama za mikono za *HATUA 10 ZA KUFIKIA ULIMWENGU WAKO ULIOPOTEA* na kuweza kusema kwa kila mtu wakati wowote.

**Utangulizi:**

- Pitia *HATUA* 8 za kwanza: Acha wasikilizaji warudie *HATUA* hizo kwako pamoja na ishara za mkono kwa kila moja.

- Wakati wewe na timu yako mnapokusanya waumini wapya kwenye mmea mpya wa kanisa, ni muhimu kudumisha harakati za **kuzidisha** — kwamba kila mwanafunzi ni mwanafunzi **anayezidisha**, na kila kanisa ni kanisa **linalozidisha**. Unafanya hivyo kwa kurudia *HATUA* 8 za kwanza za*HATUA 10 ZA KUFIKIA ULIMWENGU WAKO ULIOPOTEA*.

## HATUA 9: ZIDISHA WANAFUNZI

ZIDISHA wanafunzi walio katika kanisa jipya kwa kurudia tena hatua hizo 8 za mwanzo. (1 Wathesalonike 1:7-8)

**KUJIZIDISHA HADI KIZAZI CHA 4**

1. Kujizidisha hadi Kizazi cha 4 ndiyo ufunguo wa kueneza Injili kwenye jamii yako kwa kuwa ndiyo inayoleta kujizidisha kwenye faida.

2. Kujizidisha kunafuata mkakati wa vizazi vinne wa 2 Timotheo 2:2.
   - **Kizazi 1**: **Paulo** alifundisha
     - **Kizazi 2**: **Timotheo** (Na wengine wengi) alifundisha
       - **Kizazi 3**: **Watu Waaminifu** (waliokabidhiwa alichojifunza Timotheo)
         - **Kizazi 4**: **Na Wengine** (waliofundishwa na Watu Waaminifu)

3. Huu mzunguko wa kujizidisha hadi Kizazi cha 4 unatakiwa uendelee usisimame. Kila kizazi kinachofuata lazima kianze hatua ya **Kizazi cha 1** na kisha **kujizidisha** hadi **Kizazi cha 4**.

4. Kujizidisha hadi Kizazi cha 4 kutokea katika viwango vyote.
   - Wanafunzi
   - Viongozi (pamoja na wapanda makanisa)
   - Makanisa
   - Mitembeo

5. *RAMANI YA HUDUMA YA STRATEGIC IMPACT* itakusaidia kufuatilia kujizidisha hadi Kizazi cha 4.
   A. Unaweza ukawa na *RAMANI YA HUDUMA* mbali mbali kulingana na viwango tofauti (wanafunzi, viongozi/wapanda makanisa, makanisa, matembeo).
   B. Ukimaliza *RAMANI MOJA YA HUDUMA*, anza nyingine!

*Ramani ya Huduma* kwenye kurasa zinazofuata imetengenezwa ili kukusaidia wewe "kuona" mchakato wa kujizidisha na kukusaidia wewe kufuatilia namna unavyojizidisha hadi Kizazi cha 4. Tafadhali nyofoa kutoka kwenye kitabu chako, unaweza ukaiweka *Ramani ya Huduma* ndani ya Biblia yako au kwenye kitabu cha kumbukumbu ili kujikumbusha juu ya kujizidisha katika viwango vyote… na pia itakukumbusha kuwaombea wale unaowafundisha na wale (wanaume na wanawake) wanaowafundisha.


**KUMBUKA**: *Ramani ya Huduma* imetengenezwa kwa namna rahisi. Unaweza ukaiandika au kuchora hata kwa mkono kwenye karatasi yako.

**Mapendekezo ya kielelezo cha mfano kwa kuwashirikisha wanakongamano**

Unapoendelea kufundisha *Ramani ya Huduma*, chagua watu watakaojitolea kuonyesha mfano wa kujizidisha hadi Kizazi cha 4 kulingana na *Ramani ya Huduma*.

- Chagua kiongozi atakayesimama kwenye nafasi ya Kizazi cha 1. Wasimame mbele.
- Chagua viongozi 2 wasimame mbele ya watu wa Kizazi 1. Waeleze watu wa Kizazi cha 1 waweke mikono kwenye mabega ya watu wa Kizazi cha 2.
- Chagua viongozi wa Kizazi cha 3 wasimame mbele ya watu wa Kizazi cha 2, watu wa Kizazi cha 2 waweke mikono juu ya mabega ya watu wa Kizazi cha 3.
- Chagua viongozi 8 wasimame mbele ya watu wa Kizazi cha 3, watu wa Kizazi cha 3 waweke mikono juu ya mabega ya watu wa Kizazi cha 4.
- **KUMBUKA**: Hii inaonyesha kuzidisha kwa kielelezo. Badala ya ukuaji kwa kuongeza wanafunzi: 1, 2, 3, 4, 5… ukuaji wa kielelezo wa wanafunzi huenda: 1, 3, 7, 15… Hii ni kanuni nzuri ya kueneza jamii, jiji, wilaya, taifa, bara, na ulimwengu na Injili!

Ikikamilika itaonekana hivi:



**STRATEGIC IMPACT - UZINDUZI WA KIONGOZI**

## ZANA: *JINSI YA KUTUMIA RAMANI YA HUDUMA YA STRATEGIC IMPACT*

1. **Kizazi 1** — Write your name on the line in the center of the page. You are the 1st Generation multiplier.
   - Karatasi zima lina **mstatili mmoja**. Mzidishaji mmoja kwa ajili ya ufalme ambaye ni – **WEWE**. 1 = 1

2. **Kizazi 2** — Kunja hiyo karatasi mstari wa mkunjo upite katikati ya jina lako. Majina mawili ya wanafunzi utakaowafundisha (akina "Timotheo" wako) yataandikwa kwenye mistari iliyo mwanzo na mwisho wa jina lako. Hao sasa ni Kizazi cha 2 cha wanaojizidisha.
   - Sasa tuna **mistari mitatu ya mstatili** kwenye ukurasa wote kuna (wewe), na katika pande mbili za jina lako kuna Kizazi 2 cha wanaojizidisha. Sasa kuna **watu watatu** wanaojizidisha kwenye ufalme, wewe na watu wa Kizazi cha 2. 1 + 2 = 3

3. **Kizazi 3** — Kunja tena hiyo karatasi ili mkunjo upite kwenye majina ya watu wa Kizazi cha 2 wanatakiwa waanze kuwafundisha watu wa Kizazi cha 3 (**watu waaminifu**).
   - Sasa tuna **mistatili saba** katika karatasi lote upo (wewe), Kizazi cha 2 cha wanaojizidisha, na wengine sasa ni watu 7 wanaojizidisha kwa ajili ya ufalme – wewe, Kizazi cha pili na wa nne wa Kizazi cha 3! 1 + 2 + 4 = 7

4. **Kizazi 4** — Endelea na mchakato na Kizazi cha 4(na wengine) wakati huo huo Kizazi cha 3 cha wanaojizidisha wakitiwa moyo na kufundishwa .
   - Ramani yako ya huduma inapokuwa imejazwa mistari yote hadi Kizazi cha 4 utakuwa na jumla ya **wanaojizidisha 15** kwa ajili ya ufalme! 1 + 2 + 4 + 8 = 15


Tulipoanza kulikuwa na mstari mmoja tu uliokuwa umejazwa. Mzidishaji mmoja kwa ajili ya ufalme **WEWE**. Lakini badala ya wewe pekee yako kuongeza watu unaowafundisha, ulianza kufundisha na kufanya kazi kupitia wanafunzi wa Kizazi 2 ili na wao wawafundishe na kuwaandaa Kizazi 3. **Umezidisha** badala ya **kuongeza**! Hukuendelea tu kuwa na "watoto katika imani" lakini pia uliwaandaa hao waamini wapya kuwa na "watoto katika Imani" kwa ajili yao sasa wewe umekuwa babu/bibi wa kiroho. Kwa hiyo umekuwa babu/bibi wa hiroho wa Kizazi cha 3 cha wanaojizidisha. Na Kizazi cha 4 wameletwa katika Imani na kufundishwa na Kizazi cha 3! Hivi ndivyo **kujizidisha** kunavyofanya kazi hii ina **nguvu** kuliko **kuongeza**. Katika kila kizazi tunazidisha wazidishaji!

Kwa kutumia *RAMANI YA HUDUMA* ni rahisi kufuatilia hadi Kizazi cha 4 wakati wazidishaji ambao umewafundisha wakiendelea kujizidisha hadi Kizazi cha 4, huu mchakato utakuwa ni jambo la kawaida na kuwa sehemu ya wafuasi wa Yesu Kristo! *RAMANI YA HUDUMA* inafanya kazi katika viwango vyote vya kujizidisha- wanafunzi, makanisa, viongozi, na mitembeo kwa hiyo anzisha *RAMANI MPYA YA HUDUMA* katika kila kiwango.

Hakikisha kwamba **kila mtu** katika **kila kizazi** anaanzisha *RAMANI YA HUDUMA* (karatasi yoyote nyeupe inaweza kutumika kama *RAMANI YA HUDUMA*) ili kufuatilia kujizidisha na hakikisha kwamba inaendelea.

Huu ndiyo moyo wa *SAFARI YA MAISHA KUFIKIA ULIMWENGU WAKO ULIOPOTEA*. Utakapokutana na *TIMU YAKO YA SAFARI* ili kufanyia kazi hatua za *SARARI HATUA 1* miezi inayokuja, utajifunza namna ya kuwaongoza watu katika kumuamini Yesu na kuwafanya wanafunzi wanaojizidisha na kuzidisha wapanda makanisa- hadi Kizazi 4, utatii na kusaidia kutimiza Agizo Kuu la Yesu. Atakutumia wewe kama sehemu ya mpango wake mkuu kuufikia ulimwengu uliopotea.

# RAMANI YA HUDUMA



**MAELEZO KWA UFUPI:**

**Lengo**: Mnenaji atawahamasisha wachungaji na viongozi kujitoa na kuweka kipaumbele cha kuwafanya mataifa kuwa wanafunzi.

**Kujua**: Viongozi lazima wajue kwamba kipaumbele cha Yesu ni kufanya mataifa kuwa wanafunzi wanaojizidisha.

**Kujisikia**: Viongozi watiwe moyo na kuhamasishwa kufanya huduma zao kuwa kitovu cha kutengeneza wanafunzi wanaojizidisha.

**Mambo ya Kufanya**: Viongozi watajitoa wenyewe kuwafundisha na kuwaandaa wanafunzi wanaojizidisha.

**Utangulizi:**

- Agizo Kuu SIYO mwelekeo au mtindo mpya wa huduma. Siyo kongamano la kisasa kuja kwenye eneo lako. Agizo Kuu linatakiwa liwe MSINGI cha HUDUMA yako katika MAISHA.

- Kuna mambo mengi "mazuri" ambayo makanisa yanajishughurisha nayo. Lakini mara nyingi kanisa limesahau **huduma kuu**ambayo Yesu alitupatia kufanya – Maneno yake ya mwisho; **Agizo Kuu** linapatikana mara 5 katika Agano Jipya (Mathayo 28:18-20; Marko 16:16; Luka 24:46-49; Yohana 20:19-21; Matendo 1:8)

1. **MAMLAKA YA YESU inatulazimisha kufanya anachotaka tufanye. (**Mathayo 28:18)
   A. Yesuni Bwana mfufuka mwenye mamlaka YOTE mbinguni na duniani. Ana mamlaka juu ya mambo ya ulimwengu wa roho na ulimwengu wa mwili!

   B. Kama wanafunzi wa Yesu tunatakiwa tutii na kuyafuata mapenzi yake kama mfalme.

2. **AMRI YA YESU inafafanua tunachotakiwa kufanya.** (Mathayo 28:19-20)
   A. Amri pekee kwenye huu mstari ni **kuwafanya wanafunzi** - maandiko mengine ni maelezo ya **NAMNA** ya kuwafanya wanafunzi.

      1. **NENDENI** — Tunafanya haya pale **tunapokwenda** kwa watu mbalimbali.
         a. Kwenda ni **kuchukua hatua** ya kuwafanya wanafunzi — siyo kusubiri waliopotea kuja.
         b. Watu wengi wanaishi kwenye maeneo ambayo kuna mataifa mengi (makabila na makundi ya watu) kwa hiyo Swali hapa siyo utakwenda? Nenda kila siku. Swali halisi ni kwamba: "JE UTAKWENDA KUWAFANYA MATAIFA KUWA WANAFUNZI?"

      2. **KUWABATIZA** — Kwa njia ya **ubatizo** tunawaingiza waamini katika imani chini ya Utatu Mtakatifu.
         a. Kwenye ubatizo, ni alama ya kufa kwa utu wetu wa kale na kufufuka katika maisha mapya pamoja na Kristo (Warumi 6:4).

         b. Ubatizo ni ishara ya kuoshwa — hali ya nje inaonyesha usafi wa ndani uliofanywa kwa damu ya Yesu ili kuondoa dhambi zetu (2 Wakorintho 5:21).

         c. Ubatizo, ni alama ya kuzamishwa ndani ya Kristo na kuchukua tabia yake — kama vile kuchovya nguo kwenye rangi (dye). Nguo haiwi rangi lakini inachukua baadhi ya tabia za rangi. Tufanane na Kristo katika upendo, matendo na huduma (Wagalatia 3:27).

   d. Kwenye ubatizo, Tunatambulishwa kama sehemu ya watu wa Kristo — kanisa ni tangazo la hadharani na tamko la kuwa ni sehemu ya familia ya Mungu, mwili wa Kristo — Kanisa (Waefeso 4:4-6).

3. **KUFUNDISHA — Tunawafundisha** kutii yote aliyotuagiza.
   a. Mtu kumwamini Yesu kwa ajili ya wokovu, anakuwa amezaliwa mara ya pili kama vile mtoto mchanga, watahitaji kujaliwa kwa neema, kuwaelewa na kuwapenda.
   b. Lakini lengo siyo kuwaacha kama wachanga katika Kristo, Dhamira yetu ni kuwafundisha ili wakue ndani ya Yesu ili waweze kuzaa maisha ya Yesu kwenye maisha ya watu wengine. Ili nao waweze kujizidisha!
   c. Jambo moja wanalotakiwa kutii ni Agizo Kuu — kwenda kuwafanya wanafunzi wanaojizidisha!

B. Matokeo ya kutii Agizo Kuu ni wanafunzi wanaojizidisha — kwenda na kuwafanya wanafunzi wanaojizidisha.

C. Lengo ni kuwafanya wanafunzi wanaojizidisha katika mataifa yote (makundi ya watu na nchi) za ulimwengu.

D. Kipindi cha kazi hii ya kuwafanya wanafunzi hadi mwisho wa dahali, Amri hii ni kwa waamini wote katika vizazi vyote na usiache hadi Yesu atakaporudi.

**Agizo Kuu Ni KUWAFANYA WANAFUNZI na mambo ya kufanya lazima uyape kipaumbele katika huduma!**

3. **UWEPO WA YESU ndiyo unaotupa ujasiri unaotuwezesha kutimiza Agizo Kuu** (Mathayo 28:20).
   A. Yeye (mwenye mamlaka yote) atakuwa pamoja nasi tunapofanya yale aliyotuagiza kufanya.

   B. Uwepo wake utatuwezesha na kutupatia mahitaji yote ili kutimiza Agizo lake (2 Petro 1:3).

**HITIMISHO:**

- Haijarishi jinsi gani unakuwa katika huduma, **huwezi** "kuhitimu" kutoka kwenye huduma ya kuwafanya wanafunzi.

- Kama ukienda kwenye kiwanda cha viatu ukakuta wafanyakazi wanafanya mambo mazuri lakini hawatengenezi viatu, hicho kiwanda kitakuwa **kimeshindwa**.

- Kama wewe na kanisa lako hamuwafanyi watu kuwa wanafunzi wanaojizidisha mutakuwa hamfanyi tulichoagizwa na Kristo.

- Wewe na Kanisa lako lazimamulifanye Agizo la Yesu kuwa ni kipaumbele cha kwanza.

- *"Ambaye sisi tunamhubiri habari zake tukimwonya kila mtu, na kumfundisha kila mtu katika hekima yote, tupate kumleta kila mtu mtiifu katika Kristo. Nami najitaabisha kwa neno hili, nikijitahidi kwa kadri ya kutenda kazi kwake atendaye kazi ndani yangu kwa nguvu."* (Wakolosai 1:28-29)

**Je utajitoa katika maisha yako ili kuendelea kuwafanya wanafunzi wanaojizidisha kwa ajili ya Yesu?**

**Strategic Impact - Uzinduzi wa Kiongozi**

## Kipindi 10: *Mwaliko: Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea*

**MAELEZO KWA UFUPI:**

**Lengo**: Mnenaji ataelezea namna ambavyo *Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea* inavyoweza kuwasaidia viongozi kuanzisha mtembeo wa kuwafanya wanafunzi wanaojizidisha, viongozi na makanisa ili kumpa kila mtu fursa ya tumaini pekee la uzima ndani ya Yesu Kristo.

**Kujua**: Viongozi wataelewa kwamba tutaeneza injili kwenye miji, nchi, ukanda kwa njia ya kuzidisha wanafunzi watakaoanzisha moto wa mtembeo wa wapanda makanisa.

**Kujisikia**: Viongozi watajisikia furaha na ujasiri kupewa zana zilizothibitishwa ambazo zitawasaidia kuzidisha wanafunzi, viongozi (wapanda makanisa) na makanisa.

**Mambo ya Kufanya:** Viongozi watajitoa ili kujiandikisha kuanza *Safari* na kuzindua *Safari* kwenye makanisa yao.

**Utangulizi:**

- Mungu amekuitaWEWE kama kiongozi wa kanisa lake kutimiza Agizo Kuu kwenye mji wako, nchi, kanda n.k.

- Kama viungo katika kanisa lake tumeitwa kuwafanya wanafunzi wa mataifa yote, kuanzia mahali ulipo. Swali ni hili, "Ni jinsi gani tunampa nafasi kila mtu kwenye mji, nchi, kanda kusema ndiyo kwa Yesu?"

- Munayo hazina na rasilimali **zote** kwa ajili ya kutimiza hii misheni kubwa. Huhitaji **chochote zaidi** ya Injili, Biblia, Roho Mtakatifu na marafiki na kuungana mkono na waamini wenzio ili kuzindua mtembeo.

- Hatuhitaji mkakati au mbinu mpya. Tunatakiwa turudi nyuma kwenye mkakati wa kanisa la 1 kwenye karne 1 kwa sababu wao walifanya na kufanikiwa! Huu ndo mkakati wa *Hatua 10 za Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea*.

- Ni lazima tufuate **mfano** wa **mkakati** huu kama tunataka kuona matokeo ya namna hii kwenye miji, taifa na kanda. kuzidisha viongozi watakaozidisha wanafunzi watakaopanda makanisa yanayojizidisha.
    - **Mkakati** wa **msingi** ni: Kufanya Uinjilisti, Wanafunzi, Kufundisha, Kujizidisha.

- *Strategic Impact* imeandaa zana inayofuata mtindo huu.

1. ***Safari ya Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea [Safari]* ni zana itakayokusaidia kuendelea kuzidisha wanafunzi, viongozi, makanisa na mitembeo. Mambo ya msingi ya *Safari* are:**

    A. USHIRIKA, KUKUA KIROHONA, na KUSOMA BIBLIA: Kukua na kutumika pamoja kama ***Timu ya Safari*** **watu 3 hadi 5**. Mkutane pamoja na *Timu* yako kenye *Vituo Vya Mapumziko* pamoja na timu yako **kila wiki** ili kujifunza. Kukua, kuomba na kutumika.

    B. KUJIFUNZA: someni na kujadiliana zoezi kwa ufupi ili kukusaidia kukua katika eneo la kujiendeleza binafsi, kujiendeleza katika uongozi na kujizidisha katika huduma kwa kufuata kanuni za kibiblia.

    C. UTII wa MATENDO: Timiza wajibu wako kwa Mungu unaouweka kila wiki.

D. UNJIILISTI: Kila mwanakikundi katika *Timu ya Safari* atamshirikisha Injili angalau mtu mmoja kila wiki.

**2. *Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea* itakuwezesha kutimiza Agizo Kuu.**

A. Kuna ***Hatua* 5** za kuwaendeleza wanafunzi wanaojizidisha, viongozi, makanisa na mitembeo.

B. Kila *Hatua* inachukua **wiki 15**.

C. Mchakato wote unachukua **miaka 2 hadi 3**.

D. Mwisho wa kila *Hatua* utaamua kama Mungu anakuongoza kwenda *Hatua* nyingine au la.

**3. Kama utakuwa mwaminifu kujiandikisha katika *Safari* na kufuata mchakato wote mambo yafuatayo yatatokea:**

A. **Utakua** katika imani na kuwa kiongozi anayewafanya wanafunzi, na mpanda makanisa aliyekomaa.

B. **Utapata** marafiki na watia moyo katika *Safari* yako ya utumishi ndani ya Kristo.

C. **Utawaleta** wengine katika imani ya Bwana wetu Yesu Kristo.

D. **Utaanzisha** na **kuongeza** angalau seli moja.

E. **Utafundisha** na **kuandaa** viongozi na wapanda makanisa wanaojizidisha hadi Kizazi cha 4.

**HITIMISHO:**

◉ Hatupo hapa kufurahia kongamano zuri tu. Tupo hapa ili kuanzisha MTEMBEO ENDELEVUwa kuufikia ulimwengu kwa injili ya Yesu Kristo.

◉ **Changamoto**: Tunakupa changamoto ya kujitoa ili kuwa mwanafunzi anayejizidisha, anayesaidia kupanda makanisa (seli) na kuwafundisha wanafunzi watakojizidisha kwa kujisajiri kwenye ***Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea***.

◉ Hizi ni nyakati bora na nzuri kuishi kama mkristo. Usipoteze hizi fulsa – Jitoe kuufikia ulimwengu kwa Injili. Jiandikishe kwenye *Safari* ili kuanzisha mtembeo wa kuufikia mji, nchi, kanda na ulimwengu.

**Wape changamoto ya kuanza *Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea***
Tangaza mambo yafuatayo:

- “Tunaenda kuwa na maswali na majibu kwa ufupi kuhusiana na *Safari*. Kinachofuata baada ya kipindi hiki tutaenda kuwa na muda mchache wa maombi ili kukupa fursa wewe ya kuamua kujitoa na kujiunga na *Safari* au la. Si jambo jepesi kuamua, lakini lina matunda mengi kwenye ufalme wa Mungu kama ukiamua kujiunga!”

    - (Wewe na timu yako mruhusu maswali kutoka kwa viongozi na utoe majibu angalau kipindi cha maswali na majibu kichukue dakika 10 kisha ruhusu kipindi kifupi cha maombi kwa ajili ya busara ya kuamua kile ambacho Mungu anawaongoza kufanya.) Kisha muendelee:

- “Tatakuwa na kipindi kingine cha ziada — *Hatua 10*: Fungamanisha Mikono Pamoja Ili Kuzindua Mtembeo. Baada ya hiki kipindi tutafunga *Uzinduzi wa Kiongozi*.”

  “Wale ambao bado **hawajafanya** uamuzi wa kujiunga na *Safari* — asante kwa kuhudhuria *Uzinduzi wa Kiongozi*! Tunaamini mumebarikiwa kwa muda ambao tumekuwa pamoja. Ni matumaini yetu kwamba mtaendelea kuwafanya wanafunzi wanaojizidisha kama sehenu ya huduma yenu. tukimaliza Kipindi cha 10 basi muwe huru KUONDOKA kwa Baraka zetu! Tunawapenda na tumefurahi kuwa nanyi! Kwa wale ambao **HAWAPO** tayari kujiunga na ***Safari*, Kipindi cha 10 ndiyo mwisho wa kuwa na wewe**. **Mungu akubariki UNAPORUDI NYUMBANI. Huu ndo mwisho wa muda wetu pamoja nanyi. Tutawaachilia baada ya Kipindi cha 10.”**

  **“**Kwa wale ambao **muko tayari** kujiunga na *Safari* — tafadhali ungana nasi mara baada ya kumaliza Kipindi cha 10. Tutakusaidia namna ya kuanza mchakato wa kujiunga na *Safari* kwa kukupitisha kwenye zoezi fupi la mfano la *Vituo Vya Mapumziko*.”

**MAELEZO KWA UFUPI:**

**Lengo**: Mnenaji atapitia *HATUA 10 ZA KUFIKIA ULIMWENGU WAKO ULIOPOTEA*.
**Kujua**: Viongozi wataelewa *HATUA 10* za *HATUA 10 ZA KUFIKIA ULIMWENGU WAKO ULIOPOTEA*.
**Kujisikia**: Viongozi watajisikia uvuvio wa kuyatoa maisha yao kutimiza Agizo Kuu — au kufa wakijaribu.
**Mambo ya Kufanya**: Viongozi watajitoa maisha yao ili kuishi kutimiza Agizo Kuu la Kristo na kisha "kufungamanisha mikono" na wengine ili kuwaonyesha agano la kujitoa kufanya kazi.

**Utangulizi:**

- Pitia *HATUA* 9: Waeleze viongozi warudie kutamka hizo *HATUA* baada yako na kuonyesha alama za mikono katika kila *HATUA*.

- *HATUA* ya mwisho katika *HATUA 10 ZA KUFIKIA ULIMWENGU WAKO ULIOPOTEA* ni…

## HATUA 10: FUNGAMANISHA MIKONO PAMOJA ILI KUZINDUA MTEMBEO

FUNGAMANISHA mikono na viongozi wengine kuzindua mtembeo wa kuzidisha wanafunzi ili kutimiza Agizo Kuu

A. Pitia *HATUA 10* na alama za mikono kwa kila moja.

B. Agizo Kuu ni kubwa kwa kila mmoja wetu – linatuhitaji sisi sote kujitoa kufikia kizazi chetu kwa Injili!

C. Kwenye Kipindi chetu cha mwisho tutakupa wewe fursa ya kuingia kwenye agano takatifu pamoja na sisi, mbele za Mungu, ili kufikia kizazi chetu kwa injili ya Yesu Kristo — au kufa tukijaribu.

D. Agano ni jambo la kujitoa kwa kumaanisha, tafadhari usiingie kwenye Kipindi kinachofuata kama hujamaanisha kujitoa kikamilifu.

### *Strategic Impact - Uzinduzi wa Kiongozi*
## Kufunga: *Kufungamanisha Mikono kwa ajili ya Kuweka Agano*

**MAELEZO KWA UFUPI:**

**Lengo**: Mnenaji atawahamasisha viongozi kufanya agano ili kutimiza Agizo Kuu.

**Kujua**: Viongozi wajue kwamba wanapoeneza Injili ya Yesu Kristo wanatembea kwenye mapenzi ya Mungu.

**Kujisikia**: Viongozi watafurahi na kushawishika kujitoa kwa ajili ya kufikia kizazi hiki kwa Injili ya Yesu Kristo.

**Mambo ya Kufanya**: Viongozi watatimiza agano lao na Mungu na kwa kila mmoja kwakulifanya Agizo Kuu kuwa kitovu cha huduma zao.

1. Yesu alikuja kwa Kusudi la kuwapatanisha waliopotea pamoja na Yeye!
   - *"Kwa kuwa mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea."* (Luka 19:10)

2. Mungu Hayupo tayari kuona **MTU YEYOTE** anakosa fulsa ya kusema "Ndiyo" kwa Yesu!
   - "*Bwana hakawii kutimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu yeyote apotee, bali wote wafikilie toba.*" (2 Petro 3:9)

3. Mbinu ya Mungu kutimiza haya ni SISI Tumeitwa kutoka gizani ili tuwe katika nuru, TUTANGAZE ukuu wake katika kizazi hiki!
   - *"Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani."* (1 Petro 2:9)

4. Sisi ni mabalozi wake katika ulimwengu huu sisi ni WAWAKILISHI wake tunatakiwa kukifikia kizazi hiki kwa kuwapa tumaini la PEKEE la wokovu kwa njia ya Yesu Kristo!!!
   - *"Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kana kwamba Mungu wetu anasihi kwa vinywa vyetu; twawaombea ninyi kwa ajili ya Kristo mpatanishwe na Mungu."* (2 Wakorintho 5:20)

◉ Sisi siyo watu wa kwanza! Watu wengi waaminifu wametutangulia, nao ni pamoja na **John Knox** Mwinjilisti wa Presbyterian kutoka Scotland, ambaye alilia kwa Mungu akisema; ***"Nipe Scotland … au nife"*** Alikuwa na shauku sana ya kuona watu wake wanafikiwa na injili kiasi kwamba alikuwa tayari kuyatoa maisha yake kwa ajili ya roho zao. Mungu aliyaheshimu maombi yake yenye shauku na akamtumia John Knox sana kuhubiri katika ardhi ya kwao (**nchi yake**).

Tunawatafuta watu watakaojitoa kwa kiwango kama hicho. Tunatafuta watumishi wa Mungu wakike na wakiume watakaolia **PAMOJA NASI** wakisema "Ee Mungu ______(taja eneo, mji, nchi, Afrika)______au NIFE!"

Kama umemaanisha kwa asilimia **100%** mbele za Mungu nakuarika ufanye agano kama hilo na sisi muda huu:

**Mapendekezo ya mfano kwa kuwashirikisha wanakongamano**
Waombe viongozi waliotayari kufanya agano watengeneze mduara mkubwa, kisha wafungamanishe mikono. Kisha sema maneno ya agano yaliyopo hapa chini, baada ya hapo waongoze viongozi kufanya agano kwa pamoja.

**"Bwana, kwa neema yako, Najitoa kwako kabisa.**
**Naomba pamoja na John Knox: 'NIPE ________________________… au NIFE!'**

**"Naahidi kwako, Baba wa mbinguni, Ninayatoa maisha yangu kukifikia kizazi hiki kwa injili ya Yesu Kristo au nife nikijaribu. Kwa jina la Yesu."**

# *UZINDUZI WA KIONGOZI* ©

## *KATABU CHA MWALIMU*

## *"KUPATA UZOEFU WA AGIZO KUU"*

# *KUZINDUA SAFARI YA MAISHA KUFIKIA ULIMWENGU WAKO ULIOPOTEA* ©

***Strategic Impact - Safari ya Maisha Kuufikia Ulimwengu Ulipoptea***
## ***Kuzindua Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea***

**MAELEZO KWA UFUPI:**

**Lengo**: Mnenaji atahakikisha kwamba, viongozi wote wapya wanaojiunga na *Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea* au: **(1)** *Timu ya Safari*, au **(2)** utakusanya timu kutoka kwenye kanisa lako ili kuanza *Safari*. Viongozi wataelewe mchakato wa *Safari*, na kuanza kuhusika na *Vituo vya Mapumziko vya Timu* kila wiki kama vilivyopangwa.

**Kujua**: Viongozi wataelewa wazi wazi kuhusu *Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea* na *Mchakato wa Vituo vya Mapumziko* kila wiki.

**Kujisikia**: Viongozi watajisikia vizuri na ujasiri katika uwezo wao kuendelea na *Safari*.

**Mambo ya Kufanya**: Viongozi watapata uzoefu baada ya kujifunza zoezi la kwanza la *Vityo vya Mapumziko* kutoka kwenye *Safari*.

**Utangulizi:**

- Hizi ni siku za ajabu kuwa hai na Mungu anataka kukutumia wewe kufanya kazi yake yenye utukufu hapa duniani!

- Umechaguliwa na Mungu kama mwakilishi wake ili kukifikia kizazi hiki (Ufunuo 1:5-6).

- Kwa kuwa Roho Mtakatifu anaishi ndani yako, na kama ungekuwa mkristo pekee yako duniani, basi unayo hazina ya kueneza ufalme wa Kristo na kuufikia ulimwengu wote!

- *Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea* ni zana iliyoandaliwa ili kukusaidia kukua kiroho na kuwa mtii anayefanya kazi ya Mungu kwa kuzidisha katika viwango vyote ili kutimiza makusudi yake katika kizazi hiki.

## ***MAMBO 5 MUHIMU KATIA Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea:***

***Timu ya Safari* ya watu 3-5, wanaokutana ili *Kuangalia Mambo 4* na *Maswali 10*:**

1. **USHIRIKA, KUKUA KIROHO, NA KUSOMA BIBLIA: (ANGALIA NYUMA — Maswali 1-3)**

   a. Kueni na mumtumikie Mungu kama *Timu ya Safari*. Mkutane pamoja kila wiki ili kujifunza, kukua, kuomba na kutumika (Waebrania 10:24-25; Yakobo 5:16).
   b. Huu ndiyo moyo wa *Safari*. Ni uanafunzi wa pande mbili. Ni kutiana moyo katika upendo na matendo mema (Waebrania 10:24). Katika hali ya uwazi kwa njia ya maswali ya ya kukua kiroho tunaungama dhambi na kumweka kila mmoja katika nafasi ya kuwajibika tunapotembea na Kristo (Yakobo 5:16; Wagalatia 6:1-5). Ushirika huu haujakusudiwa kuwa taasisi ya kisheria lakini **ushirika wa kusaidiana** kuwa kila kitu Mungu anataka tuwe.

2. **KUJIFUNZA: (ANGALIA JUU — Maswali 4-5, ANGALIA NDANI — Maswali 6-7, and *MWONGOSO WA SAFARI*)**

    a. Someni na kujadiliana mafungu ya Biblia kwenye *KITUO CHA MAPUMZIKO* ili iwasaidie ninyi kukua katika kujiendeleza binafsi, kujiendeleza katika uongozi, na kujizidisha katika huduma kwa kufuata kanuni za kibiblia.
    b. Vituo *HIVI VYA MAPUMZIKO* vimetengenezwa ili kuleta hamasa ya kufikiria na kujadiliana na kumsaidia kila mmoja kukua katika kila uelewa wa **kweli ya Biblia**. Someni dhana na kisha mjadiliane maswali pamoja. Majadiliano yatawasaidia kudaka na kujifunza topiki.

3. **UTII wa MATENDO : (ANGALIA JUU — Maswali 8 and Maswali 10)**

    a. **Tekeleza mambo ya kufanya ya kila wiki**.
    b. Ukifanya haya utakua kiroho na kuwa mfuasi wa Yesu, katika uongozi, ujuzi na kuwafanya wanafunzi wanaowafikia waliopotea. *SAFARI* imetengenezwa kuanzisha mtembeo kwa kuwafanya wanafunzi wanaojizidisha watakaoongoza makanisa yanayo jizidisha. hili siyo zoezi la kutumia akili tu bali ni mabadiliko ya mtindo wa maisha.

    **KUMBUKA:** (kutoka kwenye kitabu cha *SAFARI*):
    **Neno kuhusu kujitoa na *TIMU YA SAFARI* yako…**
    Munapoendelea kukua na kutumika pamoja kwenye *TIMU YA SAFARI*, munaweza mukawa na mmoja wenu kwenye kikundi ambaye pengine hawezi kutekeleza mambo munayotakiwa kutekeleza kila wiki (usemi wa "Nitafanya", Uinjilisti, kuwafunza wengine, na kusoma Biblia). Hii inaweza kutokana na majukumu mengine ya kimaisha aliyonayo au ni tabia tu ya kutokutekeleza mambo munayo kubaliana katika *SAFARI*. Kama hivi ndivyo ilivyo tunaliacha jukumu hili kuamuruu na *TIMU YA SAFARI*. Ushauri wetu ni kwamba mtu anayesuasua kwenye *SAFARI* apewe wiki 2 au 3 ili kukamilisha mambo tunayokubaliana kufanya kila wiki, na kama atashindwa kutekeleza mambo anayotakiwa kufanya kwa muda aliopewa basi mtu huyo anaweza kuwekwa kando ili *TIMU YA SAFARI* iweze kuendelea bila yeye. Watu wa namna hii wanakaribishwa kujiunga na *TIMU YA SAFARI* wakati mwingine huko mbeleni kama wakimaanisha. Watu wanaotimiza Agizo Kuu si watu wenye akili, matajiri au watu waliosisimka tu. Watu wataotimiza Agizo Kuu ni wacha Mungu waliojiitoa na walio tayari kumtii Kristo.

4. **KUTOKA NJE: (KUTAZAMA MBELE — Swali La 9)**

    a. Mshuhudie na mfundishe angalau mtu mmoja kila wiki.
    b. Lengo letu **wakati wote** ni kuhusika katika kuwaeleza wengine jinsi wanavyoweza kuja kwa Kristo kwa imani. Jambo hili linachukua namna mbalimbali ya kufanya, kuuliza maswali ya kiroho, kushirikisha shuhuda, kuelezea jinsi Mungu alivyofanya kwenye maisha yako hivi karibuni, elezea majibu ya maombi yako, washirikishe ujumbe wa injili. Unapofanya haya utakuwa na watu waliotayari kumpokea Yesu Kristo.

5. **MAOMBI**

    a. Ombeaneni mahitaji yenu.
    b. Ombeeni mambo muliyoorodhesha, na waongoze wanafunzi chipukizi, wapanda makanisa na viongozi kutimiza Agizo Kuu.

## ***SEHEMU/MAENEO ya SAFARI YA MAISHA KUFIKIA ULIMWENGU WAKO ULIOPOTEA:***

1. ***TIMU YA SAFARI*** — Iwe na watu 3-5 waliojitoa.

2. Mikusanyiko ya ***TIMU YA SAFARI*** (inayoitwa ***VITUO VYA MAPUMZIKO***), inahusisha:

   a. **Bibla:** Someni pamoja Biblia na mtendee kazi maagizo yake.
   b. **Vitabu vya *SAFARI***
      i. ***VITUO VYA MAPUMZIKO:*** Kutaneni pamoja kila wiki ili kujadiliana *MAMBO 4* ya *KUANGALIA* kutumia *MASWALI 10*.
      ii. ***MWONGOZO WA SAFARI***: Soma na wasikilize waliokutangulia mbele katika *SAFARI*.
      iii. ***ZANA ZA HUDUMA***: vitendea kazi vitakavyo kusaidia kuwafanya wanafunzi wanaojizidisha, viongozi, na makanisa.

3. Mtindo wa maisha wa ***SAFARI*** yako — Kuyaweka kwenye matendo mambo uliyoyagundua.

**HATUA KATIKA KUANZISHA *SAFARI***

1. Kutokana na viongozi, tengeneza *TIMU YA SAFARI* ya watu 3-5 kwenye kila kikundi.

   a. Ikiwezekana wachungaji wakae kundi moja, yaani wachungaji kwa wachungaji, wanaume kwa wanaume, wanawake kwa wanawake.
   b. Kama mchungaji ataenda kuanzisha *SAFARI* na watu waliopo kanisani kwake mwingize huyu mchungaji **kwa muda** kwenye *TIMU YA SAFARI* ili wapate uzoefu wa mchakato.

2. Waelekeze *TIMU YA SAFARI* WAANDIKE MAJINA YAO na MAWASILIANO yao kwenye KITABU CHA MAFUNZO — wasisitize wakitunze vizuri kwa kuwa hivyo vitabu sasa ni vyao.

3. Waeleze *TIMU YA SAFARI* wabadirishane MAWASILIANO na wenzao kwenye *TIMU YA SAFARI* kwa ajili ya mawasiliano ya mara kwa mara.

4. Waeleze *TIMU YA SAFARI* **wakubaliane** kiwango cha maandiko ya kusoma KILA SIKU.

5. Waeleze wanafunzi wakubaliane muda na mahali pa kukutana kwenye mikutano ya *VITUO VYA MAPUMZIKO* **kila wiki**.

   a. Tunashauri kwamba *TIMU YA SAFARI* ZIKUTANE KILA WIKI IKIWEZEKANA ili kuendelea mbele na *HATUA* ya *SAFARI YA MAISHA KUFIKIA ULIMWENGU WAKO ULIOPOTEA*.

## Kia *Timu ya Safari* iteue *Mwezeshaji* (Mratibu)

Ni muhimu kuelewa kwamba **mwezeshaji** siyo mwalimu/kiongozi wa ***Timu***. **Mwezeshaji** asifundishe, asihubiri, au asionekane kama yeye ndiye "Mtaalamu" wakati wa *Vituo vya Mapumziko*. Kila mtu kwenye ***Timu*** atakuwa anajifunza, atagundua na kufanya huduma pamoja. **Mwezeshaji** ataratibu tu mikutano na kupanga ratiba za *Timu ya Safari* na kutoa ripoti ya kila mwezi kwa kiongozi wa *Strategic Impact* wa eneo.

Wajibu wa **Mwezeshaji** wa *Timu ya Safari* ni:

1. **Pamoja na wanatimu, panga siku na muda wa *Timu ya Safari*, itakapokutana.**
   *Timu ya Safari* ikutane kila wiki kwa ajili ya *Vituo* 15 *vya Mapumziko* katika kila *Hatua* ya *Safari* ili ***Mambo 4 kwa Kutumia Maswali 10***. Kama *Timu ya Safari* wataamua kuruka kipindi/siku basi siku watakayokutana waendelee walipokuwa wameishia wasiruke *Vituo vya Mapumziko*.

2. **Anzeni na kumaliza kipindi kwa muda muliokubaliana. (Waefeso 5:15-16; Yakobo 5:12)**
   Kila kipindi kichukue saa 1 au saa 1½. Mwezeshaji aanzishe kipindi kwa muda unaotakiwa na amalize kwa kuzingatia muda. Heshimu muda wa kila mtu kwa kuzingatia ratiba.

3. **Kila mwezi toa Ripoti ya "Tunda la Huduma" kila mwezi kwa kiongozi wa *Strategic Impact* wa eneo.**
   Kila mwezi wewe na timu yako mupitie tunda la huduma kila mmoja na kwa pamoja kisha matokeo yake yatumwe kwa mwakilishi wa *Strategic Impact* wa eneo. **Ripoti ihusishe**:

   a. Idadi ya viongozi wapya waliopata mafunzo kwenye *Uzinduzi wa Wanafunzi Wanaojizidisha*.

   b. Idadi ya watu wapya waliojifunza kwenye *Uzinduzi wa Kiongozi*.

   c. Idadi ya watu waliyookoka kwa kumwamini Yesu.

   d. Idadi ya makanisa yaliyoanzishwa.

   e. Idadi ya viongozi walioanza *Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea*.

**Kiongozi wa *Strategic Impact* wa eneo langu ni:**
Jina: ______________________________________________
Namba ya Simu/WhatsApp: ______________________________________
Barua Pepe: ____________________________________________

**Sasa**, liongoze kundi kwenye zoezi la **Mfano** wa ***Kituo cha Mapumziko*** ili wapate uzoefu wa mchakato wa ***Strategic Impact - Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea***

# MFANO WA KITUO MAPUMZIKO - *RAMANI YA HUDUMA: NGUVU YA KUJIZIDISHA*

**TIMU WATU 3-5** **ANGALIA 4 - MASWALI 10** **VITUO 15 VYA MAPUMZIKO**

**ANGALIA NYUMA**

1. Je umejikabidhi kwa Roho Mtakatifu na kutunza upendo wenye shauku kwa ajili ya Yesu wiki hii?

2. (**KUMBUKA**: Kwenye kila *KITUO CHA MAPUMZIKO* katika *SAFARI* kipindi kinachofuata utaulizwa. Je ulikuwa mwaminifu kusoma Biblia na kutimiza ulichotakiwa kufanya wiki hii?)

3. Je umekuwa mwaminifu kuwashuhudia waliopotea na kuwafundisha wengine? Nani hao?

**ANGALIA JUU**

Soma kwa sauti **Marko 4:26-32** na **2 Timotheo 2:2** na kisha jadilianeni maswali yafuatayo.

4. Ni kitu gani ulichokipenda au kilichokutia moyo kwenye maandiko haya?

5. Ni kitu gani kimekuchanganya au kimekufanya usijisikie vibaya kwenye maandiko haya?

**ANGALIA NDANI**

Soma kwa sauti **Marko 4:26-32** na **2 Timotheo 2:2** kisha jadilianeni maswali yafuatayo...

6. Je ni jinsi gani ufalme wa Mungu unavyoweza kukua na kujizidisha?

7. Utafanya nini ili kuwafundisha wanafunzi wanaojozidisha hadi Kizazi cha 4?

**[Someni pamoja *MWONGOSO WA SAFARI 1* ukurasa unaofuata.]**

**ANGALIA MBELE**

Soma kwa sauti **Marko 4:26-32** na **2 Timotheo 2:2** again and discuss...

8. Katika mwangaza wa hii mistari ni jambo gani la utii **utakalofanya** wiki hii? Eleza kitu maalumu.

   "Nitafanya ________________________________________________________________"

9. Ni nani utakaye mshirikisha habari za Yesu na kumfundisha wiki hii (Zana zipo ukurasa wa)?

   Majina: ________________________________________________________________

   Ni kwa jinsi gani tunaweza kufanya kazi pamoja kama *TIMU YA SAFARI* katikauinjilisti na kufundisha waongofu wapya wiki hii?

10. Ni fungu gani la Biblia utakalosoma wiki hii? (Tunashauri sura 3 kwa siku)

**MAOMBI**

Munapohitimisha ombeaneni juu ya mahitaji yenu na endeleeni kuyakabidhi maombi haya kwa Bwana mpaka ***KITUO CHA MAPUMZIKO*** kinachofuata.

## Mfano wa Kituo Mapumziko - *Ramani ya Huduma: Nguvu ya Kujizidisha*

**KANUNI ya KUJIZIDISHA**
Moja ya malengo yanayoongoza *Strategic Impact* ni ya KUJIZIDISHA katika viwango vyote: Wanafunzi, Viongozi, Makanisa, Na Mitembeo. Tukiwafunza kwa ukamilifu watu wachache wanaojizidishawatasababisha jamii yote kusikia injili. Kwa namna gani?

Katika kanuni ya 2 Timotheo 2:2 ya kufikia Kizazi cha 4, "*…(**Timotheo**[2]) Na mambo yale uliyoyasikia* ***kwangu (Paul**[1]**) mbele*** *ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi* ***watu waaminifu**[3]* *watakaofaa kuwafundisha na* ***wengine**[4]*." Muhimu ni kuendelea kufanya kazi ili kuzidisha hadi Kizazi cha 4.

Zingatia mfanohuu: Ni mtindo upi wa kukua unaoweza kuuchagua?

**(A)** Kuongezeka washirika wapya 1000 kanisani kwako kila mwaka kwa miaka 20.

**— AU —**

**(B)** Kuanza na wanafunzi 2 wanaojizidisha, ukiwafundisha kila mmoja kuzaa maisha ya Yesu kwa watu wengine 2, na kila mmoja wa hao wanafunzi wajizidishe kwa watu wawili zaidi — kwa miaka 20.

**Angalia matokeo (Ukurasa unaofuata)** Kwa kutumia"**nyongeza**" ya kiroho, kutakuwa na ongezeko – na hiyo ni njema. Lakini kwa kutumia "**kujizidisha**" kiroho hilo ni kukua kunakotokana na UWEKEZAJI!

Kujizidisha KUNAONEKANA kureta matokeo **polepole** mwanzoni. Unakuwa na malengo ya kuwafundisha wanafunzi wachache kwa KINA… ili waweze kuwa *wazidishaji* waliokomaa!

Kwa njia ya ongezeko utakuwa unasimamia waamini wapya 1000 — **Wakristo wachanga** — tangu Mwanzo. Hutakuwa na **muda** wa kutosha wa kuwafundisha waamini wapya ili wawe wazidishaji waliokomaa. Hata hivyo kwa kanuni ya "**kujizidisha**", utawekeza kwa kina kwa wanafunzi wapya wawili kwa muda na wao watafanya vivyo hivyo kwa wanafunzi wao wazuri… na vivyo hivyo kwa wanafunzi wao wapya n.k.

***Ramani ya Huduma*** (Jinsi ya kutuma *Ramani ya Huduma ya Strategic* ukurasa wa…)
*Ramani ya Huduma* ukurasa wa … imetengenezwa kukusaidia wewe "kuona" mchakato wa kujizidisha na kukusaidia wewe kufuatilia namna unavyojizidisha hadi **Kizazi cha 4**. Tafadhari nyofoa hiyo karatasi kwenye kitabu au andaa mojawapo kutoka kwenye karatasi nyeupe ihifadhi *Ramani yako ya Huduma* kwenye Biblia au kwenye daftari lako la kumbukumbu ili ikukumbushe kuombea wale unaowafundisha na wale wanaowafundisha

**KUJIZIDISHA HADI KIZAZI CHA 4**
Ni muhimu kwako wewe na wale unaowafundisha kuendelea kujizidisha hadi **Kizazi cha 4**. Hakikisha kila mtu kwenye **kila kizazi** anaanzisha *Ramani yake ya Huduma* (Karatasi lolote jeupe laweza kutumika kutengeneza *Ramani ya Huduma*) ili kufuatilia mazidisho na kuhakikisha kwamba yanaendelea.

Huu ndo moyo wa *Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea*. Utajifunza kuwaongoza watu katika imani kwa Yesu na kuwaandaa waumini wapya kufanya hivyo hivyo – kuwafanya wanafunzi wanaojizidisha na viongozi wanaojizidisha hadi **Kizazi cha 4**! Utatii Agizo Kuu la Yesu. Atakutumia wewe kama sehemu ya mpango wake wa kuufikia ulimwengu wa Injili!


**Kweli ya Msingi:** KITU UNACHOTAKIWA KUKIFANYA ILI KUTIMIZA AGIZO KUU NI KUHAKIKISHA KILA MWANAFUNZI ANAENDELEA KUJIZIDISHA HADI KIZAZI CHA 4.

[**Rudi ukurasa wa nyuma ili kujadiliana kipengele cha "KUANGALIA MBELE."**]

## Ongezeko La Kiroho au Kujizidisha?
## Matokeo — Ya Mwaka Kwa Mwaka

| | A: *(Ongezo la watu 1000 kila mwaka) Jumla ya Wanafunzi* | B: *(Anza na watu 2 na zidisha kila mwaka) Jumla ya Wanafunzi* |
|---|---|---|
| **Mwaka 1** | *1,000* | *2* |
| **Mwaka 2** | *2,000* | *6* |
| **Mwaka 3** | *3,000* | *18* |
| **Mwaka 4** | *4,000* | *54* |
| **Mwaka 5** | *5,000* | *162* |
| **Mwaka 6** | *6,000* | *486* |
| **Mwaka 7** | *7,000* | *1,458* |
| **Mwaka 8** | *8,000* | *4,374* |
| **Mwaka 9** | *9,000* | *13,122* |
| **Mwaka 10** | *10,000* | *39,366* |
| **Mwaka 11** | *11,000* | *118,098* |
| **Mwaka 12** | *12,000* | *354,294* |
| **Mwaka 13** | *13,000* | *1,062,882* |
| **Mwaka 14** | *14,000* | *3,188,646* |
| **Mwaka 15** | *15,000* | *9,565,938* |
| **Mwaka 16** | *16,000* | *28,697,814* |
| **Mwaka 17** | *17,000* | *86,093,442* |
| **Mwaka 18** | *18,000* | *258,280,326* |
| **Mwaka 19** | *19,000* | *774,840,978* |
| **Mwaka 20** | *20,000* | *2,324,522,934* |

# RAMANI YA HUDUMA





STRATEGIC IMPACT INTERNATIONAL

*"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye. Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu."*

Yoahna 3:16-18

**Kutoka kwa mistari hii, unajifunza nini kuhusu...**




FUNGA

**Sala ya imani:** *"Bwana Yesu, nakuhitaji. / Ninakiri kwako kwamba nimetenda dhambi dhidi yako na ninastahili hukumu ya milele. / Asante kwamba ulikufa na kufufuka ili kusamehe dhambi zangu zote. / Ninakuomba unisamehe na unipe uzima wa milele. Amina."*

**Je, kwa dhati uliweka imani yako kwa Yesu kukusamehe dhambi zako na kukupa uzima wa milele? Una nini sasa? (1 Yohana 5:11-12)**

Huu ni mwanzo wa maisha yako mapya na uhusiano wako na Mungu. Tungependa kukutana nawe tena ili kuzungumzia kutoka katika Biblia jinsi unavyoweza kukua katika uhusiano wako na Mungu. **Je, tunaweza kukutana lini kesho?**

Wakati ________________ Mahali ________________________________

FUNGA


Wakati ________ Mahali ____________________

Vidokezo

*"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye. Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu."*

Yoahna 3:16-18

**Kutoka kwa mistari hii, unajifunza nini kuhusu...**




FUNGA

**Sala ya imani:** *"Bwana Yesu, nakuhitaji. / Ninakiri kwako kwamba nimetenda dhambi dhidi yako na ninastahili hukumu ya milele. / Asante kwamba ulikufa na kufufuka ili kusamehe dhambi zangu zote. / Ninakuomba unisamehe na unipe uzima wa milele. Amina."*

**Je, kwa dhati uliweka imani yako kwa Yesu kukusamehe dhambi zako na kukupa uzima wa milele? Una nini sasa? (1 Yohana 5:11-12)**

Huu ni mwanzo wa maisha yako mapya na uhusiano wako na Mungu. Tungependa kukutana nawe tena ili kuzungumzia kutoka katika Biblia jinsi unavyoweza kukua katika uhusiano wako na Mungu. **Je, tunaweza kukutana lini kesho?**

Wakati ________________ Mahali ________________________________

FUNGA

Wakati ________ Mahali ____________________

Vidokezo

Jina ______________________ Simu ____________________

Anwani ________________________________________________

1. **Mungu anakupenda na anataka uwe na uzima wa milele pamoja Naye.**

- **2 Petro 3:9** - *"Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba."*
- **Warumi 5:8** - *"Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi."*

2. **Watu wote wametengwa na Mungu kwa sababu ya dhambi zao.**

- **Warumi 3:23** - *"... kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu."*
- **Warumi 6:23** - *"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu."*
- **2 Wathesalonike 1:8-9** -*Yesu atarudi... "katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu; watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake;."*

3. **Mungu alimtoa Mwanawe pekee mkamilifu ili afe badala yako ili kulipia dhambi zako.**

- **2 Wakorintho 5:21** - *"Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye."*
- **Yohana 14:6** - *"Yesu akamwambia, 'Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi.'"*

4. **Ni lazima uamini (weka imani yako) kwa Yesu kama njia pekee ya kukusamehe dhambi zako na kupata uzima wa milele.**

- **Yohana 1:12** - *"Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake."*
- **Waefeso 2:8-9** - *"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu."*
- **Warumi 10:9-10** - *"Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu."*

5. **Ukimtumaini Yesu pekee kama mwokozi wako anakupa uzima wa milele.**

- **1 Yohana 5:11-12** - *"... Na huu ndio ushuhuda, ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu umo katika Mwanawe. Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima."*

STRATEGIC IMPACT INTERNATIONAL

www.StrategicImpactInternational.com

© Permission to copy with attribution

3 Arrows Hope & Life Tool v3.0

Jina ______________________ Simu ____________________

Anwani ________________________________________________

1. **Mungu anakupenda na anataka uwe na uzima wa milele pamoja Naye.**

- **2 Petro 3:9** - *"Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba."*
- **Warumi 5:8** - *"Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi."*

2. **Watu wote wametengwa na Mungu kwa sababu ya dhambi zao.**

- **Warumi 3:23** - *"... kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu."*
- **Warumi 6:23** - *"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu."*
- **2 Wathesalonike 1:8-9** -*Yesu atarudi... "katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu; watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake;."*

3. **Mungu alimtoa Mwanawe pekee mkamilifu ili afe badala yako ili kulipia dhambi zako.**

- **2 Wakorintho 5:21** - *"Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye."*
- **Yohana 14:6** - *"Yesu akamwambia, 'Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi.'"*

4. **Ni lazima uamini (weka imani yako) kwa Yesu kama njia pekee ya kukusamehe dhambi zako na kupata uzima wa milele.**

- **Yohana 1:12** - *"Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake."*
- **Waefeso 2:8-9** - *"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu."*
- **Warumi 10:9-10** - *"Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu."*

5. **Ukimtumaini Yesu pekee kama mwokozi wako anakupa uzima wa milele.**

- **1 Yohana 5:11-12** - *"... Na huu ndio ushuhuda, ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu umo katika Mwanawe. Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima."*

STRATEGIC IMPACT INTERNATIONAL

www.StrategicImpactInternational.com

© Permission to copy with attribution

3 Arrows Hope & Life Tool v3.0

# SI

## Zana ya Ukuaji na Kuzidisha

V3.0

STRATEGIC IMPACT INTERNATIONAL

S.L.P. 78640 · Dar es Salaam, Tanzania
www.StrategicImpactInternational.com

© Jisikie huru kunakili na SI inayohusishwa

# Hatua 5

1. **HUSIKA**: Waulize wanaendeleaje na tafuta yaliyojiri katika maisha yao tangu mlipo achana kwenye mkutano wenu wa mwisho.
2. **TIA MOYO**: Anza muda wako kujibu maswali ya Ukuaji wa Kiroho (kulingana na Wagalatia 5: 22-23). **Wiki hii…**
   - A. *Je! Umejitiisha kwa Roho Mtakatifu na kudumisha upendo wa shauku kwa Yesu?*
   - B. *Je! Umetembea kwa upendo, amani, uvumilivu, fadhili, na msamaha katika uhusiano wako na familia, marafiki, waamini wenzako, majirani, na maadui?*
   - C. *Je! Umekua katika upendo wako na kujitolea kwa Kristo wiki hii? Vipi?*
   - D. *Je! Ulijidhibiti na kumheshimu Kristo katika shughuli zako za kifedha?*
   - E. *Je! Ulijidhibiti mwenyewe juu ya mawazo na matendo ya ngono, na tabia yoyote ya uraibu?*
   - F. *Je! Ulikuwa mwaminifu kuwashuhudia waliopotea na kuwafuata wengine? WHO?*
   - G. *Je! Ulikuwa mwaminifu kukamilisha usomaji wako wa Biblia na ahadi za "NITATAKA" wiki hii?*
3. **JADILI**: Soma na jadili kifungu cha Biblia mlichokuwa mmepeana mlipokutana kwa kufuata mfumo wa maswali 6 yafuatayo.
4. **MPANGO**: Pataneni kipengele cha maandiko matakatifu mtakayosoma wiki ijalo. (imependekezwa sura 3 kwa siku).
5. **OMBA**: Malizia muda wenu wa kukutana kwa maombi ya pamoja mkiombeana kila mtu na mwenzie na kuomba mipango mlioifikia kutokana na mswali ya 5 na 6.

## Ziara za Msingi

**1:** Yesu ni nani?
*Yohana 14:1-11*

**2:** Maisha Mapya na Upendo wa Mungu.
*Yohana 3:1-18*

**3:** Uwe na uhakika wa wokovu wako.
*Yohana 10:27-30*

**4:** Kukaa ndani ya Yesu.
*Yohana 15:1-11*

# Maswali 6

Mmoja na asome kifungu husika kwa sauti wakati wengine wanasikiliza au wanasoma wakifuatilia tokea kwenye Biblia.

Uliza maswali mawili ya awali na waruhusu waendelee kujadiliana na kupeana mawazo:

1. *Umepanda nini kutoka kwenye kifungu hiki?*
2. *Kitu gani hujapenda, au umeona kina changanya, kuhusiana na habari au kifungu hiki?*

Kusoma kifungu tena. Kujadili ijayo maswali mawili:

3. *Je, wewe kujifunza kuhusu watu kutoka katika kifungu hiki?*
4. *Je, wewe kujifunza kuhusu Mungu kutoka katika kifungu hiki?*

Baada ya muda wa majadiliano, mmoja asome kifungu kile kwa mara ya tatu kwa sauti na kisha jadilianeni maswali ya mwisho:

5. *Kulingana na kifungu hiki maisha yako yanawezaje kubadilika wiki hii? Uwe dhahili tambua. (Andika majibu ya watu na kisha mtakapokutana tena waulize maendeleo yao kulingana na majibu yao haya.)*
6. *Unamfahamu na mwingine anayehita kujua hadithi au kifungu hiki? (Taja jina, na sema kwa nini na lini utakapo mshirikisha au kumwambia.)*

## Ziara za Ukuaji na Kuzidisha

**5:** Maombi.
*Mathayo 6:5-15*

**6:** Kiri dhambi zako na kutubia.
*1 Yohana 1:5 - 2:2*

**7:** Ushuhuda wako: Waambie wengine jinsi Yesu alivyokubadilisha.
*Matendo 26*

A. Tumia hizo pointi 3 zilizoonyeshwa hapa chini fikiria kupitia ushuhuda wako mwenyewe:
   1. *Maisha yangu yalikuwaje kabla hujamwamini Yesu.*
   2. *Jinsi mlivyokutana na Yesu.*
   3. *Tofauti Yesu aliyoifanya ndani ya maisha yangu tangu nilipo mwamini Yesu.*

B. Wape na wao kushuhudia angalau dakika moja na mtu kabla hamja kutana tena safari inayokuja.

**8:** Shuhudia: Waambie wengine habari za Yesu.
*Matendo 1:1-11*
*2 Wakorintho 5:16-21*

A. Wawezeshe kutumia nyenzo za Uinjilisti za SI.
B. Nenda nao kumwambia mtu habari za Yesu kwa kutumia nyenzo hizo.
C. TAMBUA: *Kama watawaongoza watu kwa Kristo wasaidie wajifunze namna ya kutumia mwongozo ili kuwawezesha kuwafundisha na kuwalea wale walioamini wapya.*

**9:** Jiunge kwenye faragha.
*Matendo 2:40-47*
*Waebrania 10:19-25*

A. Karibisha mfuasi mwanafunzi wako kuhudhuria seli au kanisa la nyumb la nyumbani.
B. Msaidie huyu mwanafunzi kujithibitisha kuwa mshiriki wa seli.

**10:** Ubatizwe.
*Matendo 8:26-38*
*Mathayo 28:19*
*Matendo 2:40-41*

A. Karibisha mwamini mpya apate kubatizwa.
B. Mpatie nafasi mwamini huyo mpya kukaribisha familia na marafiki *(hasa wale wasio mjua Kristo)* ili washuhudie ubatizo wake.

**11:** Meza ya Bwana.
*Luka 22:14-20*

A. Mkaribishe mwamini mgeni ashiriki pamoja na wewe na wengine meza ya Bwana.

**12:** Utii.
*Yohana 14:15-21*

A. Waulize ni eneo gani la maisha wanahisi Bwana anawauliza watu.

---

**13:** Muda wa faragha, Maombi, kusoma na kujifunza Biblia.
*Luka 5:15-16*

A. Mfanye mwamni mpya atenge muda kila siku wa kusoma Biblia na kuomba.

**14:** Wasamehe wengine.
*Mathayo 18:21-35*

A. Waulize Kama kuna mtu maalumu wanayepaswa kumsamehe.

**15:** Nyenyekea kwenye Ubwana wa Kristo kunyenyekea kuna uhuru wa siri ya Mungu.
*Warumi 14:5-12*

**16:** Makusudi ya Mungu juu ya maisha yako.
*Mathayo 28:18-20*
*2 Wakorintho 5:17-21*

**17:** Injili ni nini?
*1 Wakorintho 15:1-8*

**18:** Ndoa na Familia.
*Efeso 5:22 - 6:4*

**19:** Tembea katika Roho Mtakatifu.
*Wagalatia 5:16-26*

**20:** Utambulisho wake katika Kristo.
*Warumi 6*

**21:** Kipaumbele cha upendo.
*1 Yohana 4:7-21*

**22:** Mamlaka ya neno la Mungu.
*2 Timotheo 3:14-17*

**23:** Uwakili wa maisha.
*Luka 19:10-27*

**24:** Vita vya kiroho.
*Efeso 6:10-18*

# MSIMAMO WA IMANI

## MUNGU

*Mwanzo 1:1; Kumbukumbu 6:4; Mathayo 28:19; Yohana 4:24, 10:30; 2 Wakorintho 13:14*

Tunaamini kwamba kuna Mungu mmoja wa kweli, Mtakatifu, aishiye milele katika nafsi tatu. Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, kila mmoja akiwa na sifa za umungu na tabia za uungu sawa sawa. Hapo mwanzo Mungu aliumba ulimwengu kutokuwa bila kitu na vitu vyote vilivyomo, hivyo anaonyesha utukufu wa nguvu yake, hekima na uzuri kwa nguvu yake kuu anaendelea kutunza uumbaji wake kwa utoaji wake wa mahitaji, anafanya kazi siku zote za kihistoria kutimiza makusudi yake ya ukombozi.

## YESU KRISTO

*Mathayo 20:28; Mtendo 4:12; Warumi 5:10; 2 Wakorintho 5:18-19; 1 Yohana 2:2*

Yesu Kristo ni nafsi ya pili ya milele katika utatu Mtakatifu ambaye aliungana na asili ya kweli kwa kutungwa mimba kimuujiza na kuzaliwa na bikira. Aliishi maisha ya utii mtakatifu kwa Baba na Mwana kujitoa kwa hiari yake mwenyewe aligharamia (alilipia) dhambi za wote kwa kifo chake msalabani kwa niaba yao, hivyo kutosheleza haki ya Kimungu na utimilifu wa wokovu na uzima wa milele kwa wote wanao mwamini yeye tu. Alifufuka katika wafu katika mwili ule ule pamoja na kuwa utukufu, ambao ndani yake aliishi na kufa. Alipaa mbinguni na ameketi kuumeni kwa Baba tokea huko mpatanishi na Mungu na sisi anaendelea kutuombea walio wake. Atarudi tena duniani yeye mwenyewe na ataonekana kwa macho, kuikamilisha kihistoria na mpango wa Mungu na milele.

## ROHO MTAKATIFU na MAISHA YA KIKRISTO

*Yohana 15:26, 16:8-11*

Ushirika na asili uhusiano wa kweli mnaokolewa Yesu Kristo ni maisha ya utakatifu na utii unaopatikana kwa wanaoamini kadiri wanavyo jinyenyekesha ndani yao utambuzi wa uhitaji wao wa mkombozi na kuwafanya kwa upya {anawapa maisha mapya} Wakati wa kuokolewa Roho hufanya makao ya daima ndani ya kila anayeamini ili awe asili ya utakatifu, nguvu na hekalu, na kipekee kabisa humpatia tokea ndani kila aaminiye vipawa na karama za kuyaelewa na kuyafanyia kazi maandiko. Nguvu yake na ukimwezesha Mkristo kuishi katika mwongozo wa maisha yenye kufanana na tabia ya Kristo na kuzaa matunda ya utukufu wa Baba.

## BIBLIA

*2 Timotheo 3:16; 2 Petro 1:21*

Msingi mkuu wa imani yetu ni Biblia, inavyotengenezwa kwa vitabu sitini na sita (66) katika Agano la kale, na Agano jipya tunaamini kuwa maandiko haya yanatokea katika asili ya Mungu mwenyewe na ikiletwa kwetu kupitia wateule wachache kama vyombo vilivyo chaguliwa. Hivyo basi maandiko kwa wakati mmoja na wakati huo huo yanaongea kwa mamlaka ya Mungu na yanaonyesha uwepo wa mwanadamu, kimtindo na matamshi haya na bila kukosea katika maandiko ya asili. Ni maandiko maalum, kanuni na mamlaka ya mwisho, juu ya kila jambo la imani na utii, na hakuna maandiko mengine yaliyovuviwa na Mungu kama ilivyo maandiko ya Biblia.

## WOKOVU

*Warumi 3:23; 5:8; Waefeso 2:1, 8-9*

Kusudi kuu la ufunuo wa Mungu katika maandiko ni kuwaita watu wote tupatanishwe kuwa na ushirika naye. Tangu asili ya mwanadamu alimweka kuwa na ushirika alichagua kuendelea njia yake binafsi, na hivyo aliondolewa mbali na Mungu na kuteseka kwa waka... asili yake alivyomfanya ashindwe kumpendeza Mungu. Anguko la mwanadamu lilitokea mwanzo wa kihistoria ya mwanadamu, na kila mmoja tangu wakati huo amepata taabu itokanayo na anguko hilo na hivyo anahitaji neema ya Mungu iokoayo. Wokovu wa mwanadamu, hivyo basi ni mkamilifu wa kazi ya neema ya bure toka kwa Mungu na sio matokeo kwa ujumla au sehemu ya kazi ya mwanadamu au matendo yake mema, na neema hii haina budi kupokelewa kwa imani katika ngazi ya binafsi. Mungu anapoingiza kazi ya wokovu ndani ya moyo wa mtu, anatoa uthibitisho wa Neno wake kwamba ataendelea kufanya hivyo mpaka siku ya kutwaliwa.

## HATIMA ya MWANADAMU

*1 Wathesalonike 4:16-17; Waebrania 9:27*

Kifo hufumbua hatima ya milele ya kila mtu. Kwa ajili watu wote kutakuwepo na ufufuo wa mwili katika ulimwengu wa roho na huduma itakayopelekea hatima ya kila mmoja kama hali ya kuadhibiwa ya milele kwa wale wasiookoka na maisha ya milele yenye Baraka kwa waliookoka. Wale waliomwamini Kristo utapokea ushirika wa milele na Mungu na watazawadiwa kwa kazi walizofanya katika maisha yao.

## KANISA

*Matendo 2:42; Warumi 12:1-6*

Matokeo ya kuungana na Yesu Kristo ni kwamba wale waaminio wanakuwa sehemu ya mwili wake yaani kanisa, kuna kanisa moja la kweli ulimwenguni likitokana na wote wamwaminio Yesu Kristo mwokozi na Bwana wao, maandiko yanaweza amuru wamwaminio wote kukutana pamoja na kutumia muda huo kuabudu, kuomba kufundisha neno, kutunza ubatizo na ushirika kadiri kumbukumbu zinapotengenezwa na Yesu Kristo, ushirika kwenye mwili kupitia maendeleo na utumiaji wa vipawa na karama, na kuwafikia wengine ulimwenguni. Popote watu wa Mungu wanapokutanika mara kwa mara kwa utii wa amri hii, huu ndio mwonekano wa kanisa. Wakiwa chini ya uongozi kufanya kazi pamoja katika upendo na umoja, wakimwadhimisha na kumwinua Kristo kwa utukufu wa Mungu, na ukamilifu wa Agizo Kuu la Kristo.

## IMANI na MATENDO

*1 Wakorintho 10:24, 31; 2 Timotheo 3:16-17*

Maandiko ndio mamlaka ya mwisho katika kila jambo la imani na matendo. Tunatambua kuwa imani na matendo hayawezi kumfunga ufahamu wa watu maeneo ambayo maandiko hayasemi kitu. Lakini kila aaminiye akaongozwe maeneo hayo na Bwana, ambae kila mume au mke mwisho wa siku atawajibika — atatoa hesabu kwake.

**STRATEGIC IMPACT**
*S.L.P. 78640, DAR ES SALAAM, TANZANIA*
*WWW.STRATEGICIMPACTINTERNATIONAL.COM*
© Haki zote zimehifadhiwa na Strategic Impact.
Huruhusiwi kufanya mabadiliko yoyote ya maudhui yaliyomo kwenye kitabu hiki.